# HOTUBA YA WAZIRI WA KILIMO NA USHIRIKA MHE. PAUL P. KIMITI (MB), WAKATI AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MATUMIZI YA FEDHA

# KWA MWAKA 1998/99

## I. UTANGULIZI

1. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu sasa likae kama Kamati ya Matumizi, ili liweze kujadili na hatimaye kuidhinisha Makadirio ya Wizara ya Kilimo na Ushirika kwa kipindi cha mwaka 1998/99.

2. Mheshimiwa Spika, kabla sijatoa maelezo juu ya hali ya kilimo, mifugo na ushirika nchini, naomba nitumie nafasi hii kumshukuru na kumpongeza Waziri Mkuu, Mheshimiwa Frederick Sumaye (Mbunge) kwa hotuba yake nzuri ambayo imenisaidia sana mimi kutoa ufafanuzi wa masuala yanayogusa sekta mbalimbali, hasa sekta ya Kilimo, Mifugo na Ushirika. Vile vile napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru na kuwapongeza Mawaziri wenzangu wawili walionitangulia kwa hotuba zao ambazo zimefafanua masuala mengi ya kiuchumi na kutoa mwelekeo wa bajeti ya mwaka 1998/99.

3. Mheshimiwa Spika, utakumbuka katika kikao cha Bajeti ya mwaka jana, Waheshimiwa Wabunge 94 walichangia hoja ya Wizara yangu kwa njia mbalimbali. Hoja hizo pamoja na mabadiliko ya sera ya kijumla na za sekta zimenisaidia katika kuandaa hotuba ya Bajeti ya mwaka huu wa 1998/99. Aidha nawashukuru Waheshimiwa Wabunge na hasa Kaimu Mwenyekiti Mheshimiwa Edson Halinga Mbunge wa Mbozi na wajumbe wa Kamati ya Fedha na Uchumi ambayo ilichambua kwa undani taarifa ya Wizara yangu na kutoa maoni yanayohitaji msisitizo, hasa katika utekelezaji wa mpango wa Wizara ya Kilimo na Ushirika. Pia kwa niaba ya watumishi wa Wizara yangu, naomba kuwapongeza waheshimiwa wabunge wote walioungana nasi katika kipindi cha 1997/98 na kutoa pole na rambirambi kwa wale wote tuliowapoteza kwa njia moja au nyingine.

## Hali ya Chakula Duniani

**4.** Mheshimiwa Spika, kufuatana na taarifa za awali kutoka Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), uzalishaji wa nafaka duniani katika kipindi cha 1997/98 unatarajiwa kuwa mdogo, ukilinganishwa na uzalishaji wa kipindi cha 1996/97. Hali hii imesababishwa na mabadiliko ya hali ya mazingira, hasa kutokana na upungufu wa mvua uliofuatiwa na mafuriko kwenye maeneo mengi yaliyolimwa. Makisio ya awali yanaonyesha uzalishaji wa tani milioni 1,888 za nafaka ikilinganishwa na mahitaji ya tani milioni 1,926 kwa mwaka 1998/99.

5. Mheshimiwa Spika, nchi nyingi katika bara la Afrika, hasa nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara, zitakabiliwa na tatizo la uhaba wa chakula. Hali mbaya ya hewa, milipuko ya magonjwa, uwezo mdogo wa kununua pembejeo pamoja na ongezeko kubwa la idadi ya watu vimechangia sana kuwepo kwa upungufu wa chakula. Maeneo ya Mashariki mwa Afrika yalikabiliwa sana na ukame ambao ulipunguza uzalishaji wa chakula hasa katika nchi za Kenya, Tanzania, Uganda, Somalia na sehemu ya kusini mwa Ethiopia. Baada ya kipindi cha ukame, nchi hizi zilikabiliwa na mvua kubwa zilizonyesha na kusababisha maeneo mengi kuwa na mafuriko.

Nchi za Rwanda na Burundi ziliathirika na ukame ulioambatana na vurugu za kivita na kusababisha uhaba wa chakula. Makisio ya awali yanaonyesha kuwa nchi nyingi za SADC kwa mwaka 1997/98 uzalishaji utashuka kutokana na kupungua kwa maeneo yaliyolimwa, pamoja na uzalishaji kwa eneo kuwa mdogo ukilinganisha na

msimu wa 1996/97.  Nchi za Afrika ya Kusini, Zimbabwe, Lesotho, Botswana na Zambia zilichelewa kupata mvua, wakati nchi za Tanzania, Malawi, Zambia, Swaziland na Msumbiji zilikabiliwa na mafuriko pamoja na athari za mvua za El-nino.

## Hali ya Mazao ya Biashara

6. Mheshimiwa Spika, taarifa za hali ya uzalishaji wa mazao ya biashara kwa kipindi cha 1997/98 duniani zinaonyesha kumekuwa na ongezeko la uzalishaji wa mazao ya tumbaku, korosho na pamba.  Uzalishaji wa kahawa umeshuka kwa asilimia 8.5 kutoka magunia milioni 100.32 kwa mwaka 1996/97 hadi magunia milioni 91.79 kwa mwaka 1997/98.  Pamoja na uzalishaji kuwa mdogo hapa nchini bei za mazao ya biashara yaliyoingizwa kwenye mfumo wa soko huria imetegemea sana bei ya soko la dunia.  Kwa kipindi hiki tangu tuanze mfumo wa soko huria, bei katika soko la dunia kwa mazao ya korosho, kahawa, pamba na tumbaku zilishuka kutoka viwango vya bei za soko hilo la nje za miaka ya 1995/96 na 1996/97.  Hali hiyo ilifanya wakulima wa mazao hayo kupata bei pungufu ya miaka iliyopita. kwa mfano zao la chai, bei zilipanda kidogo sana ikilinganishwa na bei ambazo wakulima wa mazao hayo walizipata katika misimu iliyopita.

## II  MAPITIO  YA MWAKA 1997/98

7. Mheshimiwa Spika, taarifa ya utekelezaji nitakayoitoa, inaweza kwa kiasi kikubwa ikakidhi maeneo fulani tu na kuacha mengine yasubiri kutekelezwa katika kipindi hiki cha mwaka huu wa fedha 1998/99.  Nimejaribu kuelezea baadhi ya matatizo yaliyosababisha kushindwa kufikia malengo hayo.  Aidha Waheshimiwa Wabunge wanayafahamu matatizo haya vizuri na ndiyo maana walichangia kwa wingi hoja ya Wizara ya Kilimo na Ushirika.

## Mazao ya Chakula

**8.** Mheshimiwa Spika, sote tunakumbuka jinsi uzalishaji wa mazao ya chakula ulivyokumbwa na madhara mbalimbali yakiwemo mafuriko pamoja na kukatika kwa mawasiliano.  Katika msimu wa kilimo wa 1997/98, sehemu nyingi hapa nchini zilipata mvua nyingi kupita kiasi, jambo ambalo badala ya mvua hizo kuleta neema, zimeleta madhara makubwa kwa mazao, watu na mali zao.  Mheshimiwa Spika, **naomba kuchukua nafasi hii ili kuwapa pole wakulima na wafugaji wote na familia zao walioathirika na maafa haya makubwa.**  Athari katika sekta ya kilimo na mifugo zimekuwa zikijionyesha wazi kutokana na matatizo mbalimbali hasa katika upatikanaji wa chakula kwa wananchi; maandalizi ya kilimo na ukuaji wa mazao; usambazaji wa chakula cha msaada; usafirishaji na usambazaji wa pembejeo.  Madhara mengine ni pamoja na milipuko ya magonjwa, wanyama waharibifu, panya na wadudu hususan senene (Green Grasshoper), na ndege aina ya quelea quelea.  Matumizi madogo ya mbolea na magugu mengi yaliathiri utayarishaji wa mashamba pamoja na palizi.  Lakini pamoja na athari hizo, kwa upande wa mifugo, malisho yaliongezeka na kuifanya mifugo yetu iwe na afya nzuri na kuboreka kwa soko la mifugo.

9. Mheshimiwa Spika, hali ya chakula, kutokana na tathmini ya awali ilitegemewa kuwa ingekuwa nzuri, lakini kutokana na maeneo mengi kuvamiwa na nzige, viwavijeshi na quelea quelea, hali ya chakula imeonyesha kuwa itakuwa mbaya ingawa kuthibitishwa kwake kutakuja hivi karibuni baada ya kukamilika kwa zoezi la kutathmini hali hiyo.

## Mazao ya Biashara

10. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mazao ya biashara uzalishaji ulikuwa siyo wa kuridhisha katika msimu wa 1997/98 ikilinganishwa na msimu wa 1996/97 kutokana na athari za mvua za El-Nino.  Uzalishaji wa kahawa ulipungua kwa asilimia 25 ya lengo la uzalishaji wa tani 50,000; korosho kwa asilimia 25 ya lengo la tani 100,000;

tumbaku kwa asilimia 30 ya lengo la tani 47,000; Pamba kwa asilimia 50 ya lengo la tani 300,000 za uzalishaji kipindi cha 1997/98. Kwa upande wa chai kumekuwepo na ongezeko la uzalishaji ukilinganisha na msimu uliopita. Ongezeko hili lilifanya viwanda vya kusindika chai visiweze kusindika chai yote iliyozalishwa. Hivyo majani ya chai mengi yaliharibika kutokana na kukosa kusindikwa kwa wakati wake. (Tazama Jedwali Na. I)

11. Mheshimiwa Spika, moja ya maeneo ambayo Waheshimiwa Wabunge wa mikoa ya kusini waliyasemea sana ni suala la kilimo cha pamba katika mikoa yao, na Wizara yangu iliahidi kulifanyia uchunguzi suala hili. Mdudu ambaye alikuwa afanyiwe utafiti ni "Red Bollwarm" (Diparopsis castanea) ambaye ndiye Msumbiji na Afrika Kusini wanapambana naye, na kwetu sisi ni Pink Bollworm (Pectinophora gossypiella). Baada ya Mhe. Njelu Kasaka aliyekuwa Naibu wa Wizara yangu na Kamishna wa Utafiti na Mafunzo kwenda Msumbiji kulifuatilia suala hili, wameridhika kuwa mdudu huyo anafanya madhara makubwa sana nchini Msumbiji kwa zao la pamba na ametapakaa sana kwenye jimbo lote la Cape Delgado. Gharama za madawa ya kuwaangamiza wadudu hawa ni kubwa sana na sehemu nyingi Msumbiji wamekuwa wakipata hasara hadi Shs. 181,102.50 kwa hekta moja.

12. Mheshimiwa Spika, sasa hivi; wakulima wetu wa pamba wameanza kuona hasara ya kilimo hiki kutokana na gharama kubwa za kunyunyizia madawa mara 3 kwa msimu mmoja kwa mdudu wetu wa humu nchini niliyemtaja. Wakati mwingine hawatii mbolea hata kidogo kukwepa gharama. Kumwongezea mkulima mdudu mwingine wa pili, itakuwa ni kumwangusha kiuchumi. Ni kwa msingi huo sheria ya Kimataifa ya **"International Phytosanitary Convention"** inayosimamiwa na FAO ambayo Tanzania ilikwisha ridhia mkataba inatuhitaji tuwe waangalifu na kusaidia kusimamia karantini hii ili upande wetu usidhurike zaidi. La muhimu ni Wizara yangu na Waheshimiwa Wabunge wa mikoa hiyo tushirikiane na uongozi wa huko ili kutafuta mazao mengine ya biashara, mpaka hapo uwezo wa kupambana na mdudu huyo utakapokuwa umepatikana kwa gharama nafuu. Nawaomba Waheshimiwa Wabunge wavute subira kwa ombi lao hili ambalo limekuwa likijitokeza mara kwa mara.

## Mazao yasiyo Asili

13. Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa mazao yasiyo ya asili ikiwa ni pamoja na mazao ya mbegu za mafuta, mboga, matunda, maua na viungo uliathiriwa sana na ukosefu wa mbegu kutokana na ukame wa 1996/97 uliosababisha mbegu za baadhi ya mazao kukosekana kwa mwaka 1997/98 hasa mbegu za mafuta. Vile vile kutokana na athari za mvua za El-Nino, mabonde mengi yanayolimwa mboga na matunda kwa wingi, kwa mfano mabonde ya mto Ruaha, Kilombero, Ruvu na Rufiji yaliathirika na mafuriko.

Bustani za miti mama ya matunda katika vituo mbalimbali nazo ziliharibiwa sana na mvua za El-Nino. Wizara yangu iliendelea kuhimiza shughuli za utafiti na uzalishaji wa mazao haya, kwa vile yameonyesha kuwa na soko zuri na kuweza kulipatia Taifa letu fedha nyingi za kigeni. Wizara inaandaa mkakati maalumu wa kuwahamasisha wakulima. Hii ni pamoja na kutoa ushauri kuanzisha vitalu vya mboga, matunda, maua na viungo na pia kutoa mafunzo ya utaalamu wa uendelezaji wa vitalu hivyo. Bustani za miti mama zilizopo chini ya Wizara yangu zitaboreshwa ili kuongeza ubora na uzalishaji wa mazao.

## Mazao yatokanayo na Mifugo

14. Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa mazao ya mifugo uliathiriwa na mvua za El-Nino. Maeneo mengi ya malisho yalikumbwa na mafuriko na baadhi ya mifugo kupotea. Hali hii ilisababisha usafirishaji wa mifugo ya biashara kuwa mgumu. Upatikanaji wa Nyama uliathirika kutokana na mvua za El-Nino zilizosababisha mawasiliano kwa njia ya reli na barabara kukatika. Hivyo lengo la kuzalisha tani 270,000 za nyama halikuweza kufikiwa katika kipindi cha 1997/98 na badala yake ni tani 260,000 tu ndizo zilizopatikana. (Tazama Jedwali Na. II).

15. Mheshimiwa Spika, shughuli za uzalishaji wa ng'ombe wa maziwa kwa mwaka 1997/98 ziliendelea vizuri, hasa kwa wafugaji wadogo wadogo wanaopata huduma kutoka kwenye miradi ya Southern Highlands Dairy

Development Project - SHDDP, Kagera Livestock Development Project - KALIDEP, Tanga Smallholder Dairy Development Project - TSDDP, World Food Programme - WFP pamoja na Heifer Project International - HPI. Jumla ya mitamba 1625 ilisambazwa kwa wafugaji. Lengo lilikuwa kusambaza mitamba 2000. Uzalishaji wa maziwa uliongezeka kutoka lita milioni 600 mwaka 1996/97 na kufikia lita milioni 670 mwaka 1997/98. Ongezeko hili lilitokana na kuimarishwa kwa vituo vya kukusanyia maziwa na kuongezeka kwa malisho.

16. Mheshimiwa Spika, baada ya Serikali kujitoa katika shughuli za uzalishaji, mashamba ya kuzalisha mitamba ya Lugufu, Nkundi, Ibaga, Sao Hill, Mivumoni na Kahama yalipimwa na kutathiminiwa kwa lengo la kubinafsishwa. Ubinafsishaji bado haujakamilika, kwa sababu baadhi ya mashamba yalikuwa hayana hati miliki (Title Deeds) na hayangeweza kutangazwa kuuzwa bila hati miliki. Aidha mifugo mingi nchini bado ni ile ya asili, ambayo hukua pole pole na hutoa maziwa na nyama kidogo. Hata hivyo mifugo hii huvumilia hali ya ukame na maradhi. Ili kuongeza ubora wa mifugo, Wizara ilianzisha vituo vya madume bora vya Butiama na Usa River-Arusha. Vituo hivi vina uwezo wa kutoa mbegu bora za ng'ombe na kuhifadhi kiasi cha dozi 150,000. Kwa sasa kituo cha Butiama hakizalishi mbegu kabisa kutokana na uhaba wa fedha. Kituo cha Usa River bado kinazalisha mbegu na hivi sasa kituo kinahifadhi mbegu zaidi ya dozi 5,000 ambazo zinatumika. Kituo hiki kina mtambo mpya wa kutoa hewa ya baridi ya Liquid Nitrogeni inayotumika kuhifadhia mbegu. Baada ya Serikali kuwaachia watu binafsi jukumu la kutoa huduma ya uzalishaji kwa chupa kumekuwepo na ongezeko la gharama za huduma hii. Hivyo wafugaji wengi sasa wanatumia madume bora, kutokana na huduma kutolingana na gharama zinazotozwa. Ili kuongeza utumiaji wa huduma za kuzalisha ng'ombe kwa chupa, Wizara yangu inaendelea kuhimiza sekta binafsi ili itoe huduma hii muhimu kwa gharama nafuu, hasa kwa wafugaji wa ng'ombe wa maziwa. Wizara ikishirikiana na sekta binafsi itaendelea kuviimarisha vituo vya madume bora ili tuweze kupata mbegu bora.

17. Mheshimiwa Spika, biashara ya zao la ngozi katika soko la nje ilishuka sana na hivyo kufanya bei za hapa nchini nazo zishuke. Hali hii pia ilichangia ukusanyaji wa ngozi uwe mdogo. Katika kipindi cha mwaka 1997/98, ngozi za ng'ombe 1,300,000, mbuzi vipande 800,000 na kondoo vipande 500,000 zilikusanywa. Lengo lilikuwa kukusanya ngozi za ng'ombe 1,500,000, mbuzi 1,000,000 na kondoo vipande 700,000. Upungufu huu ulichangiwa pia na mafuriko yaliyoharibu mawasiliano ya reli na barabara. Ngozi za ng'ombe milioni 1.0, ngozi za mbuzi vipande 860,500 na kondoo vipande 215,000, ziliuzwa nje ya nchi na kulipatia Taifa jumla ya shilingi bilioni. 3.15.

18. Mheshimiwa Spika, ili kuendeleza mbuga za malisho kwa mifugo ya asili kipindi cha 1997/98 Wizara ilikuwa na yafuatayo:-

(a) Kuendeleza mbuga za malisho kwa kuziwekea huduma bora za maji, katika mikoa ya Arusha, Singida, Shinyanga, Mara na Mbeya.

(b) Kuimarisha uzalishaji wa mbegu bora za malisho katika mashamba ya Vikuge (Pwani) na Langwira (Mbeya).

Jumla ya shs. milioni 45.5 kati ya Shs. milioni137 zilitolewa kwa ajili ya kuchimba malambo awamu ya kwanza katika mikoa ya Mbeya (2), Singida (2) Mara (2) Arusha (3) na Shinyanga (4), lakini kutokana na athari za mvua za El-Nino kazi nyingi za uchimbaji wa malambo zilichelewa kuanza na hivyo bado hayajakamilishwa. Uchimbaji wa malambo haya utakamilishwa katika kipindi cha 1998/99. Fedha za kukamilisha uchimbaji zitatolewa mara tu baada ya kupata ripoti ya utekelezaji wa awamu ya kwanza. Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wawahamasishe wafugaji ili wachangie katika uchimbaji wa malambo na kuunda kamati za malambo ili kuendeleza huduma hizo kwenye maeneo yao.

## Huduma za Ushauri kwa Wakulima na Wafugaji

19. Mheshimiwa Spika, huduma za ushauri kwa wakulima na wafugaji zimeendelea kuimarishwa kwa kutekeleza miradi ya “National Agricultural Extension Project (NAEP II)”, Southern Highlands Extension and Rural Financial Services (SHERFS)”, “Sasakawa Global 2000” na Miradi ya Uendelezaji wa Ng’ombe wa Maziwa inayotoa huduma hizo. Aidha Wizara iliendelea kushirikiana na Mashirika yanayoisaidia miradi hii yakiwemo Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB), IFAD, WFP, Serikali za Uholanzi na Uswisi. Miradi hii iliendelea kuimarisha huduma za ushauri kwa wakulima na wafugaji kwa kuwapatia wataalam vitendea kazi, kujenga nyumba za wataalam vijijini, pamoja na kutoa mafunzo kwa wataalam wa ufugaji bora, hifadhi ya ardhi na mazingira.

## Umwagiliaji

20. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa umwagiliaji, Wizara yangu iliendelea kutekeleza mpango wa muda mrefu wa kuendeleza kilimo cha umwagiliaji. Mkazo uliwekwa katika utayarishaji, usanifu, usimamiaji wa ujenzi na ukabarati wa miradi midogo midogo. Taratibu za uendeshaji wa miradi kwa wakulima na uimarishaji wa vikundi vya umwagiliaji zinaendelea. Miradi iliyotekelezwa katika kipindi cha 1997/98 ipo katika hatua mbali mbali za utekelezaji kama ifuatavyo:-

(i) Mradi wa ukarabati wa Kilimo cha Umwagiliaji wa jadi katika mikoa ya Kilimanjaro na Arusha ulikamilisha ukarabati wa sehemu muhimu za kutolea maji na kutoa mafunzo kwa wakulima, kuhusu usimamizi bora wa maji. Mradi huu unagharimiwa na UNDP.

(ii) Mradi wa Usangu umeendeleza hekta 3,000 katika vijiji 6 vilivyoko katika bonde la Usangu. Mradi huu pia unapata msaada kutoka UNDP.

(iii) Mradi wa Madibira-Mbeya (hekta 3,000) unaopata mkopo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADB) kwa asilimia 90 na Serikali kuchangia asilimia 10. Kazi ya kuhamisha mto na kujenga matuta ya kuzuia mafuriko zimekamilika, kazi zinazoendelea ni pamoja na ujenzi wa mabanio na mifereji. Aidha katika kipindi cha 1997/98 miradi mingine iliyotekelezwa kutokana na mkopo wa ADB ni Kitivo -Tanga (hekta 540) unaoendelea na Mwamapuli - Tabora (hekta 600) ambao umekamilika.

(iv) Mradi wa kuendeleza mabonde ya Mto Rufiji na Pangani unaopata mkopo kutoka Benki ya Dunia unaendelea kutekelezwa. Usanifu katika vijiji vya Ipatagwa na Lugunga (Katika bonde la mto Rufiji) na Lekitatu na Mombo (katika bonde la mto Pangani) umekamilika kwa asilimia 100. Aidha upimaji katika sehemu za Igomewo (hekta 300) na Nyamahana (hekta 160), katika bonde la mto Rufiji na Lemkuuna (hekta 400) na Soko (hekta 400) katika bonde la Mto Pangani unaendelea kukamilishwa. Shughuli za uundaji vikundi vya umwagiliaji (water users associations) na matayarisho ya mashamba ya mfano zilitekelezwa.

(v) Mradi wa uendelezaji wakulima wadogo wadogo katika mikoa yenye ukame (Tabora, Shinyanga, Dodoma, Singida na Mwanza) unaopata Mkopo kutoka IFAD umekamilika. Hata hivyo madhara ya mvua za El Nino yamesababisha kubomoka kwa mabanio (Intakes) na mifereji ya kupitishia maji ya kumwagilia. Juhudi zinafanywa ili kupata uwezekano wa kuendeleza mradi huu.

## Upatikanaji wa Pembejeo za Kilimo

21. Mheshimiwa Spika, ili kuhakikisha upatikanaji wa pembejeo, Wizara yangu kwa kupitia Mfuko wa Pembejeo za Kilimo na Mifugo katika kipindi cha 1997/98 iliwakopesha mawakala wa pembejeo jumla ya shillingi bilioni 2. Fedha hizi zinajumuisha shillingi bilioni 1 zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu mwaka jana na shilingi bilioni moja ambazo ni marejesho ya mikopo iliyotangulia. Tangu Serikali ianze kuwekeza kwenye mfuko huu, jumla ya shilingi bilioni 4.1 zimetolewa kwa wakopaji 175 nchini kote. Hata hivyo, urejeshaji wa mikopo haukuwa mzuri

kutokana na upungufu wa uzalishaji wa mazao na mifugo. Aidha mvua nyingi kupita kiasi iliharibu njia za uchukuzi na hivyo kuwafanya wasambazaji wa pembejeo wasiweze kuzifikisha kwa wakulima kwa wakati unaofaa.

22. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeendelea kuwahimiza wafanyabiashara wa mazao mbalimbali na Vyama vya Ushirika kujihusisha kikamilifu na uagizaji na usambazaji wa pembejeo. Aidha Wizara yangu imeanzisha mpango wa Taifa wa pembejeo za kahawa kwa njia ya Vocha. Mpango huu unaoendeshwa na Chama cha Kahawa nchini (TCA), ulitoa vocha zenye thamani ya shillingi bilioni 1.25 kwa wakulima wa Kahawa katika kipindi cha 1997/98. Wizara imeendelea kuwahimiza wakulima na wafugaji kujiunga na Vyama vya Kuweka na Kukopa ili waweze kujinunulia pembejeo bila kukopa kutoka mashirika au Taasisi za fedha ambazo hutoza riba kubwa. Napenda nichukue nafasi hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge, kwa kuzingatia umuhimu wa Vyama vya Ushirika, na vikundi mbalimbali (Associations) waendelee kutuunga mkono katika kuhamasisha wakulima na wafugaji ili wajiunge navyo. Hii ndiyo njia pekee itakayompa mkulima na mfugaji sauti ya pamoja ya kupambana na waagizaji pembejeo zisizo na viwango na zenye bei kubwa.

23. Mheshimiwa Spika, vile vile wafanyabiashara kwa kutumia vyanzo vyao binafsi wameendelea kuagiza na kusambaza pembejeo kwa wakulima kwa bei za ushindani. Pamoja na hayo, bei za pembejeo zimepanda sana na kuwafanya baadhi ya wakulima wapunguze matumizi ya pembejeo au wasizitumie kabisa. Makadirio ya mahitaji ya mbolea kitaifa kwa msimu wa 1997/98 yalikuwa tani 187,000 za mbolea ya aina mbali mbali. Hadi kufikia mwezi Machi 1998 zaidi ya tani 160,000 zilikwisha sambazwa sehemu mbalimbali nchini. Hata hivyo mvua za El-Nino zilizoharibu barabara na njia za mawasiliano zimeufanya usafirishaji wa mbolea kutoka mikoani kwenda kwa wakulima kuwa mgumu. Aidha katika baadhi ya maeneo nchini mbolea haikutumika ipasavyo kutokana na mvua nyingi kupita kiasi.

24. Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa madawa ya kilimo haujaweza kutosheleza mahitaji ambayo yanaongezeka mwaka hadi mwaka. Baadhi ya wafanyabiashara wameonyesha ushirikiano mzuri na wamewapatia wakulima mikopo ya madawa. Hali hii inatagemewa kuendelea kuimarika kadri uhusiano kati ya wafanyabiashara na wakulima unavyokua. Mfano, ni wanunuzi wa tumbaku ambao hutoa pembejeo za tumbaku yakiwemo madawa kwa mkopo kwa wakulima wa zao hilo. Hivyo haitegemewi kuwa na upungufu wa madawa ya tumbaku kwa sababu wafanyabiashara wanaagiza na kusambaza madawa hayo wenyewe.

25. Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tatizo kubwa ambalo limekuwa likiwapata wakulima ni pamoja na gharama kubwa za pembejeo pamoja na mabadiliko makubwa ya mara kwa mara ya bei ya mazao ya wakulima na kusababisha mkulima kutokuwa na uhakika wa kipato chake, Wizara ya Kilimo na Ushirika kwa kushirikiana na Muungano wa Vyama Vikuu vya Ushirika na Vyama Vikuu vyote inaandaa mpango wao wa kupambana na makali ya bei ya pembejeo na kuona namna ya kuweza kuanzisha mfuko wa kuhimili mabadiliko ya bei za mazao ya wakulima. Nitaomba Waheshimiwa Wabunge watuunge mkono katika maandalizi yote muhimu ya kumpunguzia mzigo mkulima.

26. Mheshimiwa Spika, kwa ujumla uzalishaji na upatikanaji wa mbegu kwa msimu wa mwaka 1997/98 haukuweza kutosheleza mahitaji. Serikali kwa kushirikiana na wahisani waliweza kununua na kusambaza mbegu za msaada kwa mikoa iliyoathirika. Jumla ya tani 6,034 za mbegu mbalimbali ziliagizwa na kusambazwa katika mikoa hiyo. Ili kufidia upungufu wa mbegu nchini kwa msimu wa 1998/99 makampuni ya CARGIL, Kenya Seed Company, PANNAR Hybreed Seeds na Zambia Seed Company walipewa vibali vya kuagiza mbegu zilizozidhibitishwa hapa nchini. Utaratibu wa kuzalisha mbegu kwa kutumia wakulima wadogo wadogo umeanza katika mikoa ya Morogoro, Dodoma na Iringa kwa majaribio. Mpango huu unaendeshwa kwa pamoja na Serikali ya Denmark.

27. Mheshimiwa Spika, upatikanaji wa zana za kilimo umeendelea kuwa chini ya mahitaji katika mwaka wa 1997/98. Sababu kubwa ya kuendelea kuwepo kwa tatizo la uhaba wa majembe ya mkono unatokana na kiwanda cha UFI kufungwa. Mahitaji ya aina mbali mbali ya majembe ya mkono katika msimu wa 1997/98 yalikadiriwa kuwa 2,500,000 wakati Kiwanda cha Zana za Kilimo Mbeya kilizalisha majembe 36,777 na wafanyabiashara

binafsi kuingiza majembe 149,984 mwaka 1997. Mahitaji ya majembe ya kukokotwa na wanyama ni 25,000 wakati yaliyopatikana ni 6,000. Matrekta yaliyopatikana ni 50 na idadi inayoagizwa inaendelea kupungua kutokana na kupanda sana kwa bei ya matrekta.

## Udhibiti wa magonjwa, wadudu na ndege na wanyama waharibifu wa mimea na mifugo

28. Mheshimiwa Spika, katika msimu wa 1997/98 Wizara yangu iliendelea na jukumu la kudhibiti uharibifu wa mazao unaosababishwa na magonjwa, wadudu (senene), wanyama waharibifu kama panya katika mashamba na maghala pamoja na ndege waharibifu wa nafaka. Wizara yangu kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Kudhibiti Nzige wa Jangwani (DLCO-EA) ilitoa ndege kunyunyizia dawa mikoa ya Dodoma, Mbeya, Singida, Shinyanga na Morogoro. Msimu wa 1997/98 udhibiti wa nzige ulifanyika baada ya wadudu hao kuonekana na kuzaliana kwa wingi katika maeneo asili ambayo ni bonde la mto Rukwa, mbuga za Iku-Katavi mkoani Rukwa, bonde la Malagarasi mkoani Kigoma pamoja na mbuga za Wembere zilizoko mkoani Tabora na Bahi Dodoma. Baada ya Wataalam kufanya savei na kuona kuwepo tishio la nzige, Wizara yangu ilisambaza lita 7,310 za dawa aina ya “Fenitrothion technical” katika maeneo yanayohusika, ndege ilikodishwa kwa ajili ya kunyunyizia dawa hiyo na kiasi cha hekta 13,300 zilizoathiriwa zilinyunyiziwa dawa.

29. Mheshimiwa Spika, Savei iliyofanywa msimu wa 1997/98 imegundua makundi makubwa ya ndege waharibifu kulingana na miaka 20 iliyopita. Makundi hayo yalionekana katika mikoa ya Mbeya, Shinyanga, Mwanza, Singida na Morogoro. Aidha ndege hawa walidhibitiwa kwa kunyunyiziwa dawa na inakadiriwa kwamba jumla ya ndege waharibifu milioni 70 (Mbeya) milioni 7.0 (Dodoma) milioni 1.0 (Shinyanga) na milioni 26.0 mkoa wa Singida waliangamizwa. Kwa sasa Savei inaendelea kufanywa katika mikoa ya Mwanza na Morogoro.

30. Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha miaka mitatu mfulululizo kuanzia 1996 panya wamekuwa ni tishio kubwa kwa Taifa. Sehemu zilizoathiriwa na baa la panya ni mikoa ya Lindi, Tanga, Morogoro na Mbeya (Chunya na Mbarali). Baada ya uchunguzi uliofanywa na wataalam, Wizara yangu ilituma kikosi cha wataalam wa panya kutoka Kituo cha Taifa cha Udhibiti wa Panya ili kusaidiana na Maafisa Kilimo, katika kuangamiza panya hao. Aidha, Wizara ilitoa nyenzo nyingine muhimu ikiwa ni pamoja na sumu ya panya kiasi cha kilo 1,500 na chambo (magunia 265 ya mahindi, mafuta ya kupikia lita 80 dagaa kilo 1,450 kwa ajili ya kutengeneza chambo) na magari 9. Pamoja na matatizo mengi yaliyojitokeza tulifanikiwa kiasi katika kazi ya udhibiti panya. Kwa mfano Mkoa wa Lindi asilimia 60 ya vijiji vyote vilivyoathiriwa vilipata chambo ambapo hekta 43,000 za mashamba zilidhibitiwa. Mikoa ya Tanga, Morogoro, Pwani na Dar es Salaam, udhibiti ulifanyika na mafanikio yalikuwa mazuri. Sehemu zote zilizohudumiwa, wakulima walifundishwa matumizi salama na tahadhari za chambo chenye sumu mashambani na ghalani. Kazi mojawapo ambayo Wizara itabidi iendelee nayo, ni kutoa mafunzo kwa wakulima wetu, popote pale walipo ili waelewe jinsi ya kupambana na baa la panya.

31. Mheshimiwa Spika, udhibiti wa magugu maji uliendelea chini ya usimamizi wa miradi ya Hifadhi Mazingira Ziwa Victoria na unagharamiwa na Benki ya Dunia. Mbinu zinazotumika ni kutumia udhibiti husishi ikiwa ni pamoja na udhibiti kibaolojia ambapo wadudu maadui wa magugu maji wapatao 22,700 wamesambazwa kwenye ziwa. Uchunguzi uliofanywa mwezi Machi 1998, umeonyesha kuwa wadudu hawa wamezaliana na kusambaa kiasi cha umbali wa zaidi ya mita 10 kutoka mahali walipowekwa. Katika maeneo haya magugu maji yanaendelea kukauka na kufa.

32. Mheshimiwa Spika,**Wizara yangu imeanzisha Kitengo cha Ukaguzi wa Mifugo** ili kudhibiti magonjwa yatokanayo na mifugo, usafirishaji mifugo na mazao yake, (Zoosanitary Inspection Unit). Madhumuni ya kitengo hiki ni kulinda afya ya mifugo kwa kudhibiti wanyama na bidhaa zitokanazo na mifugo ili kuzuia uingizaji na uenezaji wa magojwa kutoka nchi za nje. Ili kufanikisha shughuli hii, ukaguzi unafanyika ndani ya nchi, mipakani, viwanja vya ndege vya Kimataifa na bandari zote. Kuna jumla ya vituo vya ukaguzi 185 na vituo vya Karantini 19. Ukaguzi unazingatia afya za wanyama na nyaraka zinazohusiana na wanyama au bidhaa zenyewe.

33. Mheshimiwa Spika, **Ugonjwa wa Homa ya Bonde la Ufa** (Rift Valley Fever Disease) ambao huwapata

binadamu na wanyama uliripotiwa mwishoni mwa mwaka 1997 huko Kenya.  Hapa Tanzania katika mikoa ya Arusha na Kilimanjaro ulianza  mapema Januari 1998.  Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Shirika la Afya Duniani (WHO) na Shirika la Afya Muhimbili ilituma wataalam kwenda kufanya uchunguzi na ilithibitisha kwamba ugonjwa huo upo nchini. Wizara ilichukua hatua zifuatazo:-

(a) Kuwaelimisha wananchi njia za kujikinga na ugonjwa huu pamoja na kuchanja mifugo yao mapema

(b) Kuimarisha maabara zetu

(c) Kutoa semina kwa wataalam kuhusu udhibiti.

34. Mheshimiwa Spika, mwanzoni mwa mwaka 1997 maeneo ya mpakani mwa nchi jirani ya Kenya yalikumbwa na ukame ulioandamana na kuingia kwa ugonjwa wa Sotoka nchini kutokana na wafugaji kuhamahama wakitafuta maji na malisho.  Hatua za dharura zilichukuliwa kukabiliana na ugonjwa huu ambao ulionekana wilaya za Hai, Ngorongoro, Monduli na Karatu.  Jumla ya ng'ombe wapatao milioni tano na nusu (5.5m) walichanjwa katika mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Shinyanga, Dodoma na Singida.  Matokeo ya uchunguzi uliofanywa kwa kupima damu za ng'ombe  kutoka wilaya za mpakani mwa Kenya, zinaonyesha kuwa zaidi ya asilimia 90 ya ng'ombe  wamepata kinga dhidi ya sotoka.  Hivyo virusi vinavyosababisha ugonjwa huo vimeangamizwa.  Pia ufuatiliaji wa karibu unaofanywa na vituo vyetu vya **uchunguzi wa maradhi ya mifugo (VIC's) katika kanda zote pamoja na wataalamu wa mifugo wilayani na vijijini unaonyesha kwamba hakuna matokeo ya ugonjwa wa sotoka hapa nchini hivi sasa.**

35. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 1997/98, Wizara yangu iliendelea kuimarisha huduma za afya ya mifugo nchini.  Shughuli muhimu zilizotekelezwa katika kipindi hiki ni kama zifuatazo:

(a) Kuhamasisha Halmashauri zenye mifugo mingi kutenga sehemu ya mapato yatokanayo na ushuru wa mifugo kwa ajili ya kununulia madawa na kuboresha huduma za majosho. Aidha wafugaji wanahimizwa kuanzisha kamati za kuendesha majosho na pia watu binafsi wenye uwezo kumiliki majosho kibiashara.

(b) Kuimarisha, maabara kuu 7 zilizopo nchini za Temeke/DSM, Mwanza, Iringa, Mpwapwa, Tabora, Arusha na Mtwara,ili ziwe na vifaa muhimu vinavyohitajika katika kutambua magonjwa mbalimbali ya mifugo, kama vile Homa ya Mapafu (CBPP).

(c) Kusimamia shughuli za kampeni za kuzuia sotoka kwa kuwahusisha watu binafsi.  Majaribio yaliyofanywa mwaka 1997/98 kwa mara ya kwanza huko Kiteto na Moshi Vijijini yalionyesha mafanikio.

(d) Uchanjaji wa ng'ombe dhidi ya kupe na ndigana kali uliendelea vizuri, hadi Aprili 1998 jumla ya ng'ombe wa maziwa 17,500 wamechanjwa.

(e) Kampeni za kuchanja mbwa na paka ziliendelea.  Aidha Wizara imetoa mafunzo kwa wananchi pamoja na kuchanja mbwa 45,000.  Hivi sasa Wizara inazo dozi za chanjo 250,000 na kazi ya uchanjaji inaendelea.

## Utafiti wa Kilimo na Mifugo

36. Mheshimiwa Spika, utafiti wa kilimo na mifugo uliendelea kutekelezwa chini ya Mradi wa Utafiti wa Kilimo na Mifugo (National Agricultural and Livestock Research  Project - NALRP) ambao ulifikia mwisho wake mwezi Desemba 1997.  Katika kutekeleza shughuli za utafiti, mkazo umetiliwa zaidi katika kuzipa kipaumbele programu ambazo zinaweza kufanyiwa utafiti kikanda, kwa madhumuni ya kuwa na utafiti wenye gharama ndogo na ambao matokeo yake yanaweza kumsaidia mkulima katika kuongeza uzalishaji.

37. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 1997/98, vituo vya utafiti vilifanikiwa kuzalisha mbegu bora mpya za nyanya aina ya TENGERU 97 na TANYA. Tengeru 97 inapendekezwa kuzalishwa nyanda za kaskazini na za kati nchini. Mbegu hii huweza kustawi na kutoa kati ya tani 60 - 80 kwa kila hekta na vile vile haiharibiki haraka. Tanya inapendekezwa kulimwa popote nchini na inaweza kutoa kati ya tani 40 - 60 kwa hekta na pia ni nzuri kwa ajili ya kusindika viwandani. Vile vile utafiti wa maharage umependekeza aina mpya ya mbegu iitwayo JESCA. Mbegu hii huvumilia magonjwa na hustawi vizuri kwenye miinuko ya kati.

38. Mheshimiwa Spika, mwaka jana, nililijulisha Bunge lako tukufu kuwa kazi ya kutokomeza ndorobo Kisiwani Unguja iliendelea kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Nuklia na imeonyesha mafanikio makubwa. Hapajatokea maambukizo mapya ya ugonjwa wa malale wa wanyama (Animal Trypanosomiasis) tangu Septemba 1996. Naomba nichukue nafasi hii kulishukuru Shirika la Kimataifa la Nuklia kwa kugharimia mpango huo ambao umeonyesha mafanikio ya kutokomeza kabisa ndorobo Kisiwani Unguja. Baada ya mafanikio haya ya Unguja, wataalamu wataendeleza juhudi na teknolojia iliyotumika huko ili iweze kutumika kutokomeza ndorobo Tanzania Bara kwa kuanzia na Kisiwa cha Mafia.

39. Mheshimiwa Spika, pamoja na kuangamiza ndorobo, madawa ya kuzuia ugonjwa wa nagana (Bovine Trypanosomiasis) yalifanyiwa tathmini mashambani. Dawa ziitwazo “Isometamidium na Veridium” zilifanyiwa tathmini katika mashamba ya ng’ombe huko Mkwaja - Tanga kuzuia milipuko mipya ya ugonjwa wa malale ya ng’ombe. Wizara inashauri wafugaji kwenye maeneo yenye ndorobo wengi kuzitumia dawa hizo katika jitihada zao za kupambana na ugonjwa huo, wafugaji wawasiliane na waganga wa mifugo ili kupata maelekezo zaidi kuhusu dawa hizo.

40. Mheshimiwa Spika, katika juhudi za kupunguza vifo vya kuku vijijini vitokanavyo na ugonjwa wa kideri (New Castle Disease) Wizara iliendelea kufanya majaribio dhidi ya ugonjwa huo kwa kutumia aina nyingine ya chanjo ($I_2$) ya kideri isiyohitaji jokofu sawa na ile ya V4 ambayo niliarifu Bunge lako Tukufu katika hotuba yangu ya bajeti ya mwaka 1997/98. Napenda kuwafahamisha kwamba kwa matokeo ya awali ya maabara, chanjo hiyo imeonyesha kuwa na uwezo mkubwa zaidi wa kukinga kuku dhidi ya kideri kuliko chanjo ya V4. Taasisi ya Utafiti wa Magonjwa ya Mifugo - Temeke inayo mbegu ya chanjo ya ($I_2$) na punde utafiti utakapo kamilika chanjo hiyo itatengenezwa hapa nchini kama ilivyo kwa chanjo ya TECOBLAX ambayo ndiyo inayotumika kwa kinga ya ugonjwa wa Chambavu na Kimeta.

## Mchango wa Sekta Binafsi katika Utafiti

41. Mheshimiwa Spika, mikakati ya kushirikisha sekta binafsi katika kusaidia utafiti wa mazao ya biashara uliendelea kutekelezwa kwa baadhi ya mazao. Hadi Juni 1997, kiasi cha fedha kilichokuwa kimechangwa kwa ajili ya utafiti wa kuendeleza mazao mbali mbali ni kama ifuatavyo: Chai shilingi milioni 235.1, Pamba shilingi milioni 76.3, Korosho shilingi milioni 366.0, Kahawa shilingi milioni 78.9, Miwa shilingi milioni 44.0 na Shayiri shilingi milioni 10.0. Mazao mengine nayo yanaandaliwa mikakati ya kuchangia kwa madhumuni ya kuendeleza uzalishaji. Aidha uimarishaji wa uhusiano kati ya utafiti na ushauri wa kilimo bora kwa wakulima (Research - Extension Farmer Linkage) uliendelezwa katika maeneo yote nchini pamoja na kuandaa mpango wa kushirikisha uongozi wa Wilaya. Huu ndiyo mwanza wa kuanza kujitegemea sisi wenyewe katika utafiti wa mazao yetu muhimu.

## Maendeleo ya Ushirika

42. Mheshimiwa Spika, kama ilivyo katika ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi, Serikali imedhamiria kuimarisha ushirika na kupunguza kero zinazo wakabili wanaushirika na vyama vyao. Katika mwaka wa fedha wa 1997/98 Wizara ilitoa msukumo wa pekee kuhakikisha hesabu za vyama vya ushirika zinafungwa, kukaguliwa na kujadiliwa na wanachama. Vyama vya msingi takriban 4,500 vilikuwa na limbikizo la hesabu 18,000 zisizofungwa kwa wastani wa miaka minne. Kwa hiyo hesabu hizo zilipaswa kufungwa ili ziende na wakati.

Kutokuwepo kwa hesabu kunawaweka wanachama gizani kuhusu uwekezaji wa fedha zao katika ushirika kwa ngazi mbalimbali. Sababu hii ni kizuizi kikubwa kwa wananchi kupenda na kuwekeza katika ushirika. Hadi Aprili 1998 baadhi ya vyama vikuu, Apexes, na Shirikisho vina hesabu zinazokwenda na wakati. Zaidi ya nusu ya Vyama vya msingi havina hesabu zinazokwenda na wakati. Msukumo wa kufunga hesabu ni wa kudumu ili kuwezesha kufanya malinganisho ya uwekezaji kati ya wanachama na vyama vya Msingi. Pia Vyama vya Msingi na Vyama Vikuu vya Ushirika, Vyama Vikuu vya Ushirika na Apex, Apex na Shirikisho.

43. Mheshimiwa Spika, zoezi la kufunga hesabu lilikwenda sambamba na kufanya uchunguzi wa kina wa tuhuma za wizi na ubadhirifu hasa kwa ngazi za Vyama Vikuu. Uchambuzi huo ulifanywa katika vyama vikuu vya Kagera (KCU), Karagwe (KDCU), Biharamulo (BCU), na unaendelea kwa Vyama Vikuu vya Tabora (WETCU), Songea (SAMCU), Mpanda (LATCU) na Tunduru (TAMCU), Mbozi (MBOCU), Mbeya (MICU), Arusha (ACU), KNCU na SHIRECU. Wizara imegundua kuwepo kwa wizi na ubadhirifu unaofanywa na viongozi wa ushirika, hasa halmashauri na menejimenti. Wizara yangu imeshirikiana sana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya nchi, na watuhumiwa wamefunguliwa kesi kujibu mashitaka mbalimbali. Wizara itafanya hivyo kwa Vyama Vikuu vya Ushirika vyote kwa kadiri ya uwezo wake kifedha ili kupunguza wimbi la wizi na ubadhirifu katika vyama vya ushirika.

44. Chuo cha Ushirika ndiyo kitovu cha elimu, mafunzo na utafiti katika fani zote za ushirika na hupokea wanafunzi toka Afrika mashariki, kati na kusini. Lakini kutokana na hali mbaya kiuchumi na gharama kubwa za elimu na mafunzo, Vyama vya Ushirika hushindwa kutumia vizuri nafasi za masomo zilizopo chuoni (616). Katika mazingira haya, sehemu kubwa ya nafasi za masomo katika chuo hutumika kwa kozi fupi kwa walengwa mbalimbali hususan vyama vya msingi, Halmashauri na wanachama. Kwa mwaka wa fedha 1997/98, chuo kilikuwa na wanafunzi wa kozi ndefu 200 hata hivyo kimeendesha kozi fupi kwa waandishi 300, wahalmashauri 1,000 na wanachama 20,000.

45. Mheshimiwa Spika, kutokana na hali halisi msukumo wa maendeleo ya ushirika ni kwa ngazi ya vyama vya msingi. Kwa mujibu wa rekebisho la Sheria Na. 5 ya mwaka 1997, chama cha msingi kinapaswa kujenga uwezo wa kutekeleza madhumuni kiliyojiwekea. Baada ya vyama vikuu vingi kulega lega, na kutokana na huduma za wanunuzi binafsi kuwa za mashaka, wakulima wameanza kuimarisha vyama vya msingi, kwa kuchagua halmashauri wenye uwezo wa kuongoza vyama katika shughuli za biashara. Aidha wameajiri waandishi wenye muelekeo wa kutoa ushauri kiuchumi. Kwa upande wa kahawa, vyama vya msingi zaidi ya 30 kati ya 375 vinakusanya kahawa na kuisafirisha hadi viwandani, kwa kukobolewa na hatimaye kuipeleka mnadani. Kadhalika kwa zao la tumbaku, vyama vya msingi hufanya biashara moja kwa moja na wanunuzi binafsi bila kutumia vyama vikuu. Kuimarika kiuongozi kwa vyama vya msingi kutabadilisha muundo wa vyama vikuu na hata mfumo mzima wa ushirika nchini. Lakini kwa hakika kutapunguza gharama kubwa za Union kwa manufaa ya wanachama.

46. Mheshimiwa Spika, moja ya mbinu ya hakika ya kuwawezesha Watanzania wazawa kutumia rasilimali za Taifa kwa ukamilifu na ufanisi na kuondoa umaskini ni uanzishaji wa taasisi za fedha za wananchi wenyewe. Ili kufikia lengo hili Wizara yangu inatilia mkazo uanzishaji wa vyama vya Akiba na mikopo (SACCOS). Hadi Aprili 1998 vyama hivi vilikuwa na jumla ya Tshs. 6.0 bilioni katika amana na hisa, ukilinganisha na Tshs. 3.2 milioni kwa kipindi hicho hicho mwaka jana. Vyama vya Akiba na Mikopo vilitoa mikopo ya zaidi ya Tshs. bilioni 5.0 kwa wanachama kwa shughuli mbalimbali kama biashara ndogo ndogo, pembejeo, tiba, elimu, ujenzi wa nyumba. Aidha Benki ya Ushirika Kilimanjaro nayo imeendelea kujiimarisha kwa kuongeza hisa na amana. Benki hiyo ilikopesha vyama vikuu na vyama vya msingi jumla ya Tshs. 1.0 bilioni katika msimu uliopita. Huu ni ushahidi kuwa wananchi wenyewe wanayo nafasi kubwa ya kukusanya nguvu zao kwa maendeleo yao bila kuwa tegemezi.

## Mafunzo ya Wataalam na Wakulima

47. Mheshimiwa Spika, jumla ya wakulima na wafugaji 2,372 (wanawake 1,108 na wanaume 1,264) walipata

mafunzo katika fani mbalimbali za kilimo na mifugo kupitia vyuo vya Kilimo na Mifugo nchini na kuweza kuvuka lengo la kuwafundisha wakulima 2,000. Aidha wanafunzi 83 walijiunga na mafunzo ya astashahada na stashahada kwa kujigharamia wenyewe na wakati huo huo wanafunzi 173 walihitimu katika vyuo vyetu. Vile vile jumla ya watumishi 105 walipata mafunzo ya muda mfupi ndani ya nchi. Lengo letu la kuwapatia watumishi 110 mafunzo ya muda mrefu (hasa wale wenye astashahada) kwa lengo la kuinua kiwango chao cha ujuzi halikuweza kutekelezwa kutokana na uhaba wa fedha. Sambamba na hili pia Wizara haikuweza kutekeleza azma yake ya kutoa mafunzo ya muda mfupi katika fani za biashara na menejimenti ya miradi midogo midogo ya kilimo kwa ajili ya wakulima na watumishi, kutokana na ukosefu wa fedha.

## Marekebisho ya Muundo wa Wizara

48. Mheshimiwa Spika, mwaka jana nilifahamisha Bunge lako tukufu kuwa Wizara ya Kilimo na Ushirika ilikuwa inakamilisha muundo mpya kulingana na majukumu yake mapya. Muundo huo umekamilika na utaanza kutumika rasmi mwezi Julai 1998. Msingi wa marekebisho ya muundo huo ni kuwezesha kuwepo kwa mgawanyo bayana wa majukumu ya KILIMO (mazao) na MIFUGO kuwa chini ya idara mbili tofauti badala ya kuwa chini ya Idara moja. Aidha marekebisho yamezingatia hali ya sasa ya mabadiliko ya mfumo wa utendaji wa Sekta ya Kilimo katika mkoa, wilaya hadi kijijini. Wizara sasa itakuwa na Idara nne (4) na Vitengo sita (6) kama ifuatavyo: Idara ya Kilimo (mazao), Idara ya Mifugo, Idara ya Ushirika, na Idara ya Utafiti na Maendeleo. Idara hizi nne zinapewa huduma na vitengo vya Utawala na Utumishi, Uhasibu, Ukaguzi, Mipango na Sera, Hifadhi ya Chakula, na Vyuo vya Kilimo na Mifugo.

49. Aidha kutokana na mabadiliko ya muundo wa tawala za mikoa, Wizara itaimarisha ofisi za Kanda za Utafiti na kuziongezea majukumu mapya ili ziweze kuwa kiungo kati ya makao makuu ya Wizara, mikoa na wilaya. Kanda hizi sasa zitaratibu shughuli zote za kilimo, mifugo na ushirika, ikwa ni pamoja na ukusanyaji na usambazaji wa takwimu kuendeleza teknolojia rahisi kwa wakulima na wafugaji. Lengo letu kubwa ni kufikisha utaalamu kwa wakulima na wafugaji. Ofisi hizo za Kanda zipo Ukiriguru, Mpwapwa, Ilonga, Selian, Naliendele, Uyole na Tumbi. (Tazama Jedwali Na. III)

50. Mheshimiwa spikal katika kipindi cha 1997/98 Wizara yangu imeendelea kushirikiana na Tume ya Rais ya Urekebishaji Mashirika ya Umma (PSRC) katika ubinafsishaji na urekebishaji wa mashirika kama ifuatavyo: Mashamba ya Mamlaka ya Mkonge ya Ubena, Bomba, Muheza, Toronto na Kumburu yameuzwa kwa Watanzania ambapo mashamba ya Kange/Mgwisa, Ngombezi, Mruazi, Pangawe, Kitisa, Magoma, Kibaranga, Mwelya TANCORD, Tanzania Carpets Ltd. na shamba la ng’ombe wa maziwa la Ishimbu yamenunuliwa na Katani Ltd. Kampuni ya Sukari ya Kilombero imeuzwa. Viwanda vya maziwa vya Tanga, Musoma na Tabora vilivyokuwa chini ya Tanzania Dairies Ltd. viliuzwa, kile cha Dar es Salaam kilinunuliwa kwa ubia kati ya Watanzania na Wataiwani.

## Marekebisho ya Mashirika ya Umma

51. Mheshimiwa Spika, mali za biashara za Bodi ya Tumbaku ziliuzwa kwa Universal Leaf Company ya Marekani na zile za Bodi ya Pareto kwa Kampuni ya International Chemical Producers ya Afrika ya Kusini. Majadiliano na wawekezaji katika mashirika yafuatayo yanaendelea; Kampuni ya Sukari Mtibwa, Tanganyika Planting Co. Ltd., Mashamba ya kuzalisha maziwa/mitamba ya Kitulo, Rongai na Iwambi, Viwanda vya kubangua Korosho vya Tunduru, Masasi, Likombe na Tanita I. Aidha taratibu za kubinafsisha mashirika mengine zinaendelea.

## Maendeleo ya Watumishi

52. Mheshimiwa Spika, baada ya muundo wa Wizara ya Kilimo na Ushirika kukamilika, zoezi la kuhamisha Watumishi lilianza tukiwa na watumishi 13,549. Jumla ya Watumishi 7,831, waliokuwa Wizarani wamehamishiwa

Serikali za Mitaa. Watumishi 60 wamepelekwa kwenye Sekretarieti za mikoa. Aidha watumishi 400 wamepunguzwa kazi. Katika utaratibu huu Wizara imebakiwa na watumishi 5,258 ambao watafanya kazi kwenye makao makuu ya Wizara, Ofisi za Kanda na kwenye taasisi za utafiti na vyuo vya mafunzo. Watumishi waliohamishiwa Wilayani, wataendelea kupata utaalamu toka Wizarani lakini usimamizi wao utaendelea kuwa chini ya uongozi wa Serikali za Mitaa. Wizara yangu itaendelea kutunza kumbukumbu sahihi kuhusu ajira zao pamoja na kuandaa tange ya Watumishi kazini (Seniority) ili wasipoteze haki zao huko wanakohamia.

53. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 1997/98, jumla ya Watumishi 682 wamepewa ajira za kudumu na watumishi 1,966 wamethibitishwa kazini. Mpango wa mafunzo ya muda mfupi kwa baadhi ya watumishi watakaobaki Wizarani umeanza kutekelezwa. Watumishi 41 wameshapatiwa mafunzo ya kompyuta ya wiki nne katika Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam ili kuwawezesha kuitumia vyema huduma ya ukusanyaji, uchambuzi na usambazaji wa taarifa na takwimu muhimu za kilimo. (Management Information System).

## Matumizi ya Fedha za Mpango wa Maendeleo 1997/98

**54.** Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 1997/98 Wizara pamoja na mashirika yake ilitengewa jumla ya shilingi milioni 13,016.9 kwa ajili ya matumizi ya kawaida, na shilingi milioni 5,334.7 kwa ajili ya matumizi ya shughuli za maendeleo. Kati ya fedha hizo za maendeleo, shilingi milioni 560.0 ni fedha za hapa na shilingi milioni 4,774.7 ni fedha za nje. Hadi kufikia mwezi Mei, 1998 matumizi ya kawaida yalikuwa shilingi milioni 10,489.9 sawa na asilimia 80 wakati matumizi ya fedha za mpango wa maendeleo yalikuwa shilingi milioni 403.0 fedha za hapa ambayo ni asilimia 70 ya fedha za maendeleo tulizotenga.

## III MPANGO WA MAENDELEO WA MWAKA 1998/99

55. Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo kwa kirefu kuhusu maendeleo na matatizo ya Wizara yangu, yaliyojitokeza katika utekelezaji wa mpango wa mwaka 1997/98, naomba kutoa maelezo ya mpango wa maendeleo wa mwaka 1998/99. Kutokana na mabadiliko ya Sera za kijumla za uchumi na za sekta, Wizara yangu imebakia na majukumu makubwa ya kutoa huduma za ushauri kwa wakulima, utafiti na mafunzo pamoja na uandaaji na utekelezaji wa sera. Mpango wa maendeleo wa mwaka 1998/99 unalenga katika kuimarisha na kuboresha majukumu muhimu ya Wizara ya Kilimo na Ushirika kama ifuatavyo:

(a) Kuendeleza huduma ya elimu na ushauri kwa wakulima na wafugaji kwa kuzingatia mifumo ya kilimo na hali ya hewa kufuatana na maeneo na matumizi ya teknolojia ya kisasa.

(b) Kufanya utafiti wa mazao na mifugo na kusambaza matokeo ya utafiti huo haraka kwa wakulima na wafugaji.

(c) Kudhibiti magonjwa na wadudu waharibifu wa mimea na mifugo, pamoja na kusimamia kikamilifu sheria zilizopo.

(d) Kuchambua, kutayarisha na kusimamia utekelezaji wa Sera ya Kilimo, Mifugo na ya Ushirika.

(e) Kuendelea kuihamasisha sekta ya binafsi na kuishirikisha katika utoaji huduma za kilimo na mifugo.

(f) Kuimarisha ukusanyaji na uchambuzi wa takwimu na taarifa muhimu za sekta ya kilimo na mifugo na kuwahimiza waingize zana bora na za kisasa zenye unafuu kwa mkulima.

(g) Kuhamasisha uanzishaji wa vyama vya ushirika vya aina mbalimbali, pamoja na kuhakikisha ukaguzi wa mahesabu ya vyama vya ushirika unafanywa mara kwa mara na taarifa zinatolewa kwa washirika.

(h) Kuendelea kushirikiana na Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma (PSRC) katika zoezi linaloendelea la kuangalia upya miundo ya mashirika na ubinafsishaji wake.

## Huduma za Ushauri kwa Wakulima na Wafugaji

56. Mheshimiwa Spika, miradi ya huduma za ushauri kwa wakulima na wafugaji ya NAEP I na II na SHERFS itaendelea kuimarisha huduma za ushauri kwa kuwapatia wataalam vitendea kazi pamoja na kutoa mafunzo kwa wataalam na wakulima/wafugaji kuhusu kilimo na ufugaji bora. Aidha mafunzo kwa wakulima na wafugaji kupitia vipindi vya radio, vijitabu na magazeti yataimarishwa. Pia elimu kuhusu hifadhi ya mazingira na athari za kulima na kufuga kando kando na katika mabonde ya mito na vianzio vya maji itatolewa. Tathmini ya mvua za El-Nino itafanywa kwa undani mara baada ya mvua kuisha na kuweka mikakati ya kupambana na athari zake. Hii ni pamoja na kuandaa malisho ya mifugo kwa kiangazi, kulima mazao kwa kutumia unyevunyevu mabondeni wakati wa kiangazi na kuzuia mmomonyoko.

57. Mheshimiwa Spika, ingawa uzalishaji wa mbegu bora hapa nchini katika hali ya kawaida ni wastani wa tani 12,800 kwa mwaka, wakulima wengi hawatumii mbegu bora kwa sababu ya bei kubwa. Vile vile kuna tatizo la usambazaji na upatikanaji wa mbegu bora kwa wakulima kwa wakati zinapotakiwa. Wizara yangu inakamilisha na kutekeleza sera ya uzalishaji wa mbegu bora itakayo husisha wakulima wenyewe. Ili kuongeza upatikanaji wa mbegu zilizothibitishwa kwa wakulima, Wizara itaendelea kuwahamasisha wakulima wadogo wadogo, makampuni na taasisi mbalimbali katika sekta ya uzalishaji na usambazaji wa mbegu bora kushiriki zaidi. Katika kipindi cha 1998/99, mikakati ifuatayo itatekelezwa ili kuongeza uzalishaji na upatikanaji wa mbegu bora:

(a) Utaratibu wa kuzalisha mbegu kwa kutumia wakulima wadogo wadogo utaanza rasmi katika mikoa ya Morogoro, Dodoma na Iringa. Mpango huu utaendeshwa kwa kushirikiana na Serikali ya Denmark ambayo imetoa jumla ya US $ 5.0 milioni sawa na Shs. 3.3 bilioni kwa kipindi cha miaka mitano (1998 - 2002). Mpango huu wa miaka mitano, utahusika kuzalisha mbegu ambazo makampuni makubwa hayajihusishi na baadaye utaenezwa pia katika mikoa mingine. Ni matarajio ya Wizara yangu kwamba Taasisi, Makampuni na wakulima wadogo wadogo watazalisha na kuongeza matumizi ya mbegu bora kutoka asilimia 5 ya sasa na kufikia kiwango cha asilimia 50 katika kipindi cha miaka 10 ijayo. Aidha utaratibu huu utawawezesha wakulima kupata mbegu bora na kwa bei nafuu zaidi.

(b) Wizara yangu imekamilisha taratibu za kutunga **Sheria ya haki Miliki** (Plant Breeders Rights Legislation) kwa aina zote za mbegu zitakazotolewa kisheria na kamati inayosimamia mbegu bora nchini. Sheria hii italinda na kuhakikisha matumizi halali ya mbegu zote zinazotolewa na Serikali na Sekta binafsi; na kuadhibu vikali wale wote watakao shindwa kusimamia ubora wa mbegu.

(c) **Ugonjwa wa ukungu wa mahindi** 'Grey Leaf Spot' umeendelea kuwa tishio katika mikoa ya Rukwa, Mbeya, Ruvuma na Iringa. Ili kudhibiti ugonjwa huu, Wizara yangu itaendelea kuwaelimisha wakulima mbinu za kudhibiti na kuzalisha mbegu zinazostahimili ugonjwa huu. Kituo cha Uyole kinaendelea na utafiti na uzalishaji wa mbegu bora. Baadhi ya wakulima watashirikishwa katika uzalishaji wa mbegu.

## Mazao ya Biashara

58. Mheshimiwa Spika, uzalishaji wa mazao ya Biashara ambayo yanaliingizia taifa hili sehemu kubwa ya fedha za kigeni umekuwa hauongezeki kwa kasi inayotakiwa. Wizara yangu imeanza kuandaa mikakati ya muda wa kati na mrefu kwa kila zao ili kuendeleza uzalishaji. Katika msimu wa 1997/98 tumekamilisha mikakati ya kuendeleza zao la kahawa. Mikakati hiyo ni pamoja na:-

(a) Kuimarisha huduma za utafiti ili kupata mbegu bora.

(b) Kuhamasisha wakulima kutumia mbegu bora pamoja na kuimarisha huduma za ushauri.

(c) Matumizi bora ya ardhi.

(d) Kuanzisha na kuimarisha vyama vya kuweka na kukopa (SACCOS) ili wakulima wapate mikopo kwa ajili ya ununuzi wa pembejeo.

(e) Upatikanaji wa pembejeo kwa wakati unaofaa, ikiwa ni pamoja na utaratibu wa kutumia vocha.

(f) Kuimarisha soko na ubora wa zao pamoja na usindikaji.

(g) Kuangalia suala la kodi ili kuimarisha mapato ya wakulima

Mazao mengine kama korosho yanaendelea vizuri kwa kutumia fedha za mfuko wa kuendeleza zao la korosho (CIDEF) na uzalishaji unakaribia kufikia viwango vya miaka ya sabini. Kwa mwaka wa 1998/99, Wizara itaendelea kuandaa mikakati ya uendelezaji wa zao la pamba.

## Mazao yasiyo Asilia

59. Mheshimiwa Spika, mazao yasiyo asilia yakiwemo matunda, mboga, maua, viungo na mbegu za mafuta kama michikichi, alizeti karanga na ufuta yanapewa msukumo ili yaweze kuchangia kwa ukamilifu katika pato la Taifa. Uendelezaji wa mazao haya utatokana na juhudi za sekta ya binafsi. Wizara yangu itaendelea kuhimiza sekta binafsi kuongeza uzalishaji wa mazao haya na utumiaji wa huduma za kitaalam na teknolojia inayofaa ili waweze kuzalisha mazao mengi kwa eneo na yaliyo bora. Uzalishaji wa michikichi katika mkoa wa Kigoma utaendelea kupewa msukumo hasa katika kutoa huduma za ushauri wa kitaalam na kuhimiza sekta binafsi ili kuagiza mbegu bora za michikichi. Lengo ni kuongeza uzalishaji wa mafuta ya mawese kwa kutumia viwanda vyetu. Aidha Wizara yangu itaimarisha mfumo wa ukusanyaji takwimu ili kuiwezesha Wizara kufanya tathmini ya maendeleo ya Sekta hii. Kwa kufanya hivyo, Wizara itaweza pia kukusanya na kusambaza taarifa za masoko ya mazao haya ili kuunganisha masoko ya ndani na kuweza kupenya masoko ya nje.

## Umwagiliaji

60. Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa kina wa kilimo cha umwagiliaji unaonyesha kuwa Tanzania, bado inayo maeneo mazuri ambayo yanafaa kwa kilimo cha umwagiliaji. Baadhi ya maeneo haya yako katika mabonde ya mito Ruaha, Kilombero, Rufiji, Pangani, Ruvu na Wami. Hivi sasa ni hekta 175,000 tu ziko chini ya kilimo cha umwagiliaji. Mpango wa uendelezaji wa kilimo cha umwagiliaji hapa nchini umeonyesha uwezo mkubwa uliopo wa kuendeleza kilimo hiki kwa kutumia mabonde ya mito, maziwa, na mabwawa endapo itawekwa mikakati ya uendelezaji wenye uweiano mzuri na matumizi mazuri ya rasilimali tulizonazo. Mkazo ni kuendeleza kilimo cha umwagiliaji kwa kutumia wakulima wadogo wadogo, hii ni pamoja na kuhamasisha na kushauri sekta binafsi katika kuanzisha na kuimarisha ushirika wa wakulima wamwagiliaji ili kuongeza uzalishaji. Katika kipindi cha 1998/99 Wizara yangu itatekeleza yafuatayo:-

(a) Kutoa ushauri katika kuanzisha miradi midogo midogo ya umwagiliaji pamoja na kuwahamasisha wakulima kuunda vikundi na kupewa mafunzo ya namna bora ya kutumia maji mashambani (Water Users Association).

(b) Mradi wa kuendeleza kilimo cha umwagiliaji katika mabonde ya mito Pangani na Rufiji.

(c) Mradi wa Madibira na uendelezaji wa kilimo cha umwagiliaji katika maeneo ya ukame.

(d) Ukarabati wa kilimo cha umwagiliaji wa jadi katika mikoa ya Kilimanjaro, Arusha pamoja na mradi wa Kitivo.

(e) Uendelezaji wa umwagiliaji kwa wakulima wadogo nchini - (Agricultural Sector Programme Support) katika mikoa ya Morogoro, Iringa, na Dodoma.

(f) Umwagiliaji wa wakulima wadogo wadogo katika bonde la mto Wami - (Smallholder Irrigation Project in Central Wami River Basin)

(g) Uendelezaji wa Kilimo cha umwagiliaji huko Moshi chini - (Lower Moshi Intergrated Agriculture and Rural Development Project.

(h) Kusaidiana na mikoa kubuni miradi midogo midogo ambayo inaweza kuendeshwa na wakulima wenyewe.

## Maendeleo ya Ushirika

64. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itaendelea na msukumo wa kuhakikisha kuwa hesabu za vyama vya ushirika zinakamilika kwa wakati ili kutoa fursa kwa wanachama kujadili hali ya vyama vyao kiuchumi na kifedha. Kama ilivyo kwa wawekezaji wengine, wanaushirika wanatakiwa kufahamu jinsi fedha iliyowekezwa na inavyokua mwaka hadi mwaka. Wanachama wamewekeza fedha nyingi katika viwanda kama jineri, viwanda vya kukoboa kahawa n.k. kwa kukatwa kiasi fulani cha fedha kwa kilo. Lakini mwanachama mmoja mmoja hapati hati miliki yoyote kwa michango hii mikubwa na ya muda mrefu. Kwa hiyo, inapotokea mwanachama kukoma kuwa mwanaushirika kwa sababu yoyote kama uzee, halipwi chochote kinacholingana na uwekezaji huu. Hali hii ikiendelea itakatisha tamaa wakulima kujiunga na ushirika na la msingi kupunguza kasi ya uwekezaji katika vyama vyao. Kwa hiyo Wizara itaendelea kuhimiza kuwa na hesabu zinazokwenda na wakati na kufanya malinganisho ili ugavi wa mali zilizopo ulenge katika kutoa haki zaidi kwa Wanachama. Mwenendo huo mbali na kuwapa imani wanachama utaimarisha vyama na hivyo kuvutia wakulima na wafugaji kujiunga na ushirika.

65. Mheshimiwa Spika, tatizo moja kubwa kwa vyama vya ushirika ni msingi dhaifu wa mtaji na hivyo kuwa tegemezi wa mikopo kutoka vyombo vya fedha. Wakulima wadogo wadogo hawakopesheki na taasisi za fedha za biashara kwa sababu hawana kinga/dhamana. Njia moja ya kuondokana na tatizo hili ni kwa Wanaushirika wenyewe kuanzisha taasisi zao za fedha kama Vyama vya Akiba na Mikopo (SACCOS) na kujenga uhusiano wa kibiashara na benki za biashara kama National Microfinance Bank na CRDB (1996). Uzoefu tulioupata mkoa wa Kilimanjaro, wa kuanzishwa na kuendeshwa kwa Kilimanjaro Cooperative Bank (KCB) na SACCOS unaleta matumaini ya ukombozi wa mkulima mwanaushirika vijijini kwani KCB hukopesha SACCOS ambazo nazo hukopesha wanachama wake. Hivyo Wizara yangu inategemea kuimarisha SACCOS 684 zilizoko na kuanzisha SACCOS mpya zipatazo 100. Aidha Wizara yangu itasaidia Benki ya Ushirika ya Nyanza ambayo imekwisha andikishwa ili kutimiza masharti ya leseni za biashara ya fedha ili iweze kuanza kazi katika mwaka huu wa fedha.

66. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itaendeleza na kuimarisha kazi ya ukaguzi wa vyama vya ushirika ikiwa ni pamoja na kusimamia ufungaji wa vitabu vya hesabu na kutoa taarifa muhimu kwa wanachama. Ukaguzi wa SACCOS utapewa kipaumbele zaidi kwani wananchi watawekeza fedha katika vyama hivyo kama kutakuwa na uhakika wa usalama wa fedha zao. Chuo cha Ushirika Moshi kitaendelea kuwa kitovu cha elimu na mafunzo ya ushirika. Chuo kitaweka mkazo mkubwa kwa mafunzo ya muda mfupi kwa wanachama, halmashauri na wafanyakazi ili kuinua ujuzi wa kuongoza vyama. Hususan kazi za "wajibu wa Mwandishi wa Chama cha Ushirika" (PSW) na "utunzaji wa vitabu vya hesabu" (Elementary Book-keeping) kwa ajili ya waandishi wote 4,500 wa vyama. Vilevile Halmashauri wote wa vyama hivyo watasomea kozi za "Kozi za Halmashauri" na "Jinsi ya kusoma Mizania". Kozi hizo nne zitafunzwa kwa utaratibu wa Elimu kwa njia ya Posta. Aidha COASCO itaendelea kuwa taasisi muhimu ya ukaguzi wa vyama vya ushirika nchini. Kwa mwaka huu wa fedha, COASCO itatilia mkazo mkubwa kukagua vyama vya msingi hasa SACCOS ambazo hupokea fedha nyingi kutoka kwa

wanachama.

## Utafiti wa Mazao ya Kilimo na Mifugo

67. Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilika kwa awamu ya kwanza ya Mradi wa National Agricultural and Livestock Research Project - NALRP hapo Desemba 1997, Wizara yangu itaendelea kushirikiana na Benki ya Dunia na Wafadhili wengine katika kutekeleza utafiti wa kilimo na mifugo chini ya awamu ya pili mradi wa Kitaifa wa Tanzania Agricultural Research Project - TARP II. Katika kipindi cha 1998/99, chini ya Mradi wa TARP II, mkazo zaidi utawekwa katika kutatua matatizo yanayozikabili taasisi na vituo vya utafiti nchini. Umuhimu utawekwa katika kuimarisha Taasisi za utafiti (Research Institutional Development), kupata programu za utafiti zenye kipaumbele kitaifa na kikanda pamoja na kuimarisha rasilimali za utafiti na uongozi (Resource Development and Management).

68. Mheshimiwa Spika, katika kusaidia kutatua matatizo yanayowakabili wakulima na wafugaji ili kuongeza uzalishaji wa mazao na mifugo shughuli zifuatazo zitapewa umuhimu;

(a) Kuweka sawa majukumu ya Idara ya Utafiti na Maendeleo baada ya kuanzisha Baraza la Taifa la Utafiti wa Kilimo (National Agricultural Research Council).

(b) Kuundwa kwa kamati za utafiti kwenye Kanda ambazo zitakuwa na wawakilishi kutoka watumiaji mbali mbali wa matokeo ya utafiti wa kilimo na mifugo.

(c) Kutafiti aina bora za mbegu za mazao ya chakula na biashara zenye kutoa mavuno mengi na kuhimili magonjwa na ukame kulingana na vipaumbele vilivyowekwa Kikanda.

(d) Kutafiti mbinu bora na za gharama nafuu za kudhibiti wadudu waharibifu wa mimea na mifugo, pamoja na kudhibiti magugu sugu ya mazao, hasa striga kwenye mashamba ya mpunga, mahindi na mikunde.

(e) Kuendeleza utafiti wa ng’ombe bora aina ya Mpwapwa (Mpwapwa Breed) kwa nia ya kuuza mitamba kwa wafugaji wadogo wadogo hasa wale wa ng’ombe wa maziwa.

(f) Kuendeleza utafiti wa chanjo ya kideri isiyohitaji jokofu ($I_2$), kwa madhumuni ya kupunguza vifo vya kuku vijijini.

(g) Kuendeleza teknolojia rahisi ya kilimo kwa kuhimiza matumizi ya zana za kukokotwa na ng’ombe au punda.

(h) Kuhamasisha wawekezaji na wafanyabiashara binafsi waagize zana muafaka za kilimo (kama majembe ya ng’ombe; trekta ndogo na axil za mikokoteni) ili kuimarisha na kuboresha matumizi ya zana bora na za kumrahisishia kazi mkulima na hasa mwanamke kijijini.

(i) Kuimarisha mpango mzuri wa kuratibu misaada ya wahisani kwenye kanda za utafiti kwa sekta ya kilimo na mifugo.

(j) Kuhamasisha sekta binafsi kushiriki katika kuchangia gharama za utafiti, katika mazao ya mkonge na pareto pamoja na kukamilisha taratibu za kuchangia mazao ya tumbaku na shayiri.

## Udhibiti wa magonjwa ya wanyama, wadudu waharibifu wa mimea na mifugo

69. Msheshimiwa Spika, katika msimu huu 1998/99 Wizara yangu itahakikisha udhibiti wa ndege waharibifu

unafanywa kwa wakati muafaka. Aidha, Wizara yangu itahakikisha zoezi la kuangamiza makundi ya nzige ambao hawajawa na uwezo wa kuruka unafanyika mapema na vile

vile kutoa mafunzo kwa ajili ya wataalam kwenye zoezi la udhibiti wa nzige. Aidha tatizo la panya limekuwa kubwa sana kwa msimu wa 1997/98, ukilinganisha na misimu iliyopita. Wizara yangu itaendelea kuwafundisha wakulima namna ya kutabiri kutokea na kudhibiti mlipuko wa panya hasa sehemu ambazo hazikufikika kwa ajili ya kukosa mawasiliano. Wataalam wa kilimo na mifugo vijijini watafundishwa namna ya kutabiri kutokea kwa mlipuko wa panya na kutumia mikakati ya udhibiti husishi (Integrated Pest Management), kwa vile wataalam wa kituo cha udhibiti wa panya Morogoro ni wachache.

70. Mheshimiwa Spika, ili kudhibiti tatizo la magugu maji, katika msimu wa 1998/99, Wizara yangu kwa kushirikiana na ofisi ya Makamu wa Rais inategemea kujenga vituo 3 vitakavyozalisha wadudu wa magugu maji katika mikoa ya Kagera, Mwanza na Mara; kuendelea na usambazaji wa wadudu hao katika sehemu zote zenye magugu maji; kuelimisha wananchi kuhusu mbinu zote zitakazotumika katika udhibiti wa magugu maji pamoja na kushirikisha wananchi waishio kando ya ziwa katika uvuaji wa magugu maji.

71. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu itaimarisha mikakati ya kuzuia na kudhibiti kikamilifu magonjwa ya milipuko ili kuzuia hasara inayoweza kuletwa na magonjwa hayo na gharama kubwa ya kuyadhibiti iwapo yatatokea. Wizara itaendeleza juhudi za kupambana na kichaa cha mbwa na homa ya Bonde la Ufa, kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Maliasili na Utalii. Katika kipindi cha 1998/99 Wizara itaweka umuhimu zaidi katika kuimarisha uwezo wake wa kuzuia mifugo yenye ugonjwa au inayotiliwa mashaka kuwa na ugonjwa kwa kuwekewa Karantini ili kuzuia kuenea kwa magonjwa ya mifugo. Wizara inategemea kuchanja mbwa 300,000 dhidi ya kichaa cha mbwa na ng’ombe 300,000 dhidi ya homa ya Bonde la Ufa. La muhimu zaidi, Wizara itajitahidi kutoa mafunzo ya msingi juu ya tiba kwa wafugaji wenyewe, ili kazi za kawaida za kumtibu mnyama, waweze kuzifanya.

## Upatikanaji wa Zana na Pembejeo za Kilimo

72. Mheshimiwa Spika, ili kuboresha huduma ya upatikanji wa pembejeo za kilimo, Wizara yangu itaendelea kuhamasisha na kuhimiza wafanyabiashara na taasisi nyingine kuagiza na kusambaza pembejeo. Aidha Wizara yangu itaendelea kuwahimiza wakulima wajiunge na vyama vya kuweka na kukopa ili kuwawezesha kukusanya rasilimali kwa ajili ya kununulia pembejeo. Kwa upande wa kahawa, Wizara yangu itaimarisha mpango wa kununua pembejeo za kahawa kwa kutumia Vocha. Mpango huu umeanzishwa ili kuwawezesha wakulima kununua pembejeo za kahawa bila kutumia pesa taslimu. Aidha Wizara yangu itakiimarisha kitengo cha Pembejeo ili kiweze kuratibu na kudhibiti ubora wa pembejeo. Sambamba na juhudi hizi, Wizara yangu inazifanyia marekebisho sheria za pembejeo ili kuwa na sheria moja inayosimamia pembejeo zote. Hili litasaidia kuadhibu wale wote wanaoingiza pembejeo ambazo ni chini ya viwango vinavyotakiwa kisheria. Pamoja na hilo Wizara itaendelea kuhimiza kutumia mbolea asilia zikiwemo samadi, mboji na malejea ili kurutubisha ardhi. Mwaka huu wa fedha Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 1.0 kwa ajili ya mfuko wa pembejeo. Kutokana na fedha zitakazorejeshwa, mfuko unatarajia kukusanya marejesho ya shilingi bilioni 2.0. Ili pamoja na hizi zilizotengwa mwaka huu mfuko uweze kutoa mikopo itakayofikia shilingi bilioni 3.0.

## Kilimo cha Zana

73. Mheshimiwa Spika, karibu asilimia 70 ya wakulima nchini hulima kwa kutumia jembe la mkono, asilimia 20 hulima kwa kutumia jembe la kukokotwa na ng’ombe na asilimia 10 tu ya Watanzania hutumia kilimo cha trekta. Hii inatokana na uwezo mdogo wa wananchi kuweza kununua zana bora za kilimo ambazo zingeweza kutumika ili kuongeza mapato. Ili kuendeleza na kuimarisha teknolojia rahisi Wizara yangu inahimiza upatikanaji wa zana bora za kilimo na vifaa kutoka sekta binafsi ili kutosheleza mahitaji ya wakulima kwa bei nafuu. Hivi sasa Wizara inahimiza uingizaji wa trekta ndogo ndogo na zana zake ambazo zina uwezo wa kulima hekta 10 hadi 15 kwa msimu. Serikali ya Japan kupitia KR II itasaidia pia katika suala hili ili kueneza zana hizi. Aidha Wizara

itaendelea kuzingatia yafuatayo ili kuimarisha teknolojia ya kilimo bora:-

(a) Wizara itaendelea kuhimiza utumiaji wa wanyama wa kukokota zana kwa ajili ya kilimo na usafirishaji pamoja na kuimarisha huduma, ushauri na za tiba ya mifugo hasa malisho ya mifugo.

(b) Wizara itahimiza sekta binafsi ili kuanzisha na kuendesha vituo vya kukodisha matrekta ili kulima na kupanda kwa wakati muafaka, pamoja na matumizi bora ya pembejeo za kilimo kama mbegu na mbolea.

(c) Wizara itaanzisha muundo bora wa kutoa taarifa kuhusu vitendea kazi, vifaa bora vya kilimo na mashine za kisasa zinazowapunguzia wakulima na wafugaji hasa kina mama adha kubwa ya kazi na wakati huo huo kuwaongezea kipato.

(d) Kuimarisha ushauri kwa wakulima kwa kuhamishia wataalamu karibu nao. Pia mafunzo kwa wakulima na uimarishaji wa mashamba ya majaribio kwa kueneza teknolojia mpya inayotolewa na vituo vya utafiti vya Wizara.

(e) Kuhamasisha uanzishaji wa vyama vya kuweka na kukopa (SACCOS) vya wakulima ili viwezeshe kununua pembejeo na zana za kilimo. Tatizo kubwa la mkulima ni uwezo duni wa kifedha katika kuendeleza kilimo chao.

(f) Kueneza huduma za umwagiliaji katika sehemu zote ambazo zina maji ya kumwagilia ili kuepukana na tatizo la kutegemea mvua za msimu.

74. Katika kutekeleza azma ya Serikali ya kuingia karne ya Sayansi na teknolojia, jitihada za Wizara zimeanza kwa kuhusisha mikoa miwili ya Morogoro na Dodoma kuanza mwaka huu wa mpango wa kueneza teknolojia rahisi katika baadhi ya vijiji kwa kutumia wawekezaji binafsi ambao mtaagiza zana rahisi na za kurahisisha kazi za shambani chini ya msaada wa FAO. Katika awamu hii ya majaribio, kiasi cha Tshs. milioni 170.0 zimetolewa na Shirika la Chakula Duniani (FAO) kuendeleza azma hiyo. Awamu nyingine itategemea mafanikio ya mikoa hiyo miwili.

Katika kuhimiza pia watumiaji wa fedha za Serikali za “Import Support” tumekwisha wasilisha mapendekezo yetu kwa Waziri wa Fedha kuwa fedha hizo kwa sekta ya kilimo zitolewe kwa watu wanaotarajia kuingiza zana bora za kisasa zenye teknolojia rahisi na nyepesi kwa wakulima wetu, badala ya mtindo wa kila mmoja wao kuagiza bidhaa ambazo hazimwendelezi mkulima kiteknolojia. Mfano wa matrekta madogo; plau na axils za mikokoteni, na vipuli vya matrekta ambayo yamesimama kutokana na ukosefu wa vipuli.

## Mafunzo ya Wataalam na Wakulima

75. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 1998/99 Wizara yangu itaendelea kutilia mkazo mafunzo ya wakulima na wataalam kwa lengo la kuwapatia mbinu na teknolojia bora ili kuendesha kilimo cha biashara. Wizara pia itaendelea kuhamasisha wafadhili wa ndani na nje ya nchi katika kugharamia mafunzo kwa ajili ya watumishi wao. Aidha vyuo vitaendeleza juhudi za kujitangaza pamoja na kuweka mazingira yatakayovutia wanafunzi, ili wajiunge na mafunzo yenye manufaa kwao. Kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kilimo na Chakula (FAO), Wizara yangu itaangalia kwa kina mahitaji ya utaalamu wa kilimo na ufugaji katika kutoa ajira ya uhakika vijijini (gainful rural employment) na kudumisha uendelezaji wa kilimo (sustainable agricultural development). Matokeo ya utafiti huu yatasaidia Serikali kupanga mikakati ya kuendeleza kipato na kutoa ajira vijijini na kupunguza wimbi la vijana kukimbilia mijini kutafuta ajira. Kwa mwaka wa 1998/99, Wizara pia ina mpango wa kuwapatia mafunzo wakulima na wafugaji 2500. Aidha Wanafunzi 120 watakaojigharamia katika vyuo vyetu nao watapewa mafunzo.

## Maendeleo ya Watumishi

76. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 1998/99 Wizara yangu inatazamia kuwasilisha TUMEAJIRI mapendekezo ya kupandishwa vyeo watumishi wapatao 1,852, hao ni pamoja na 1,224 ambao hawakupanda kwenye kipindi hiki kutokana na agizo la kusitisha zoezi la kupandisha vyeo. Baadhi ya watumishi hao ni wale waliohamia TUMITAA. Zoezi hili ni muhimu ili kuwahakikishia wale wote waliohamia TUMITAA kuwa ajira yao inalindwa pamoja na kuwa wamehama.

77. Mheshimiwa Spika, mpango wa Wizara yangu kutoa mafunzo kwa Wakuu wa Idara, Wahasibu, Maofisa Utumishi na Makatibu Mahsusi umekamilika. Mafunzo hayo yatahusu "Human Resource Management", Stores, Uhasibu, na" Office Management practices". Mafunzo haya yanasubiri uteuzi wa Wakuu wa Idara na watumishi wengine kwa mujibu wa muundo mpya ili mafunzo yatolewe kulingana na shughuli za mtumishi.

## Marekebisho ya Mashirika ya Umma

78. Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilika kwa muundo mpya wa Wizara kulingana na majukumu yake mapya, Wizara yangu itaendelea kuzifanyia marekebisho sheria zinazohusu sekta za mazao, mifugo na ushirika ili kuipatia sekta binafsi mazingira mazuri ya kushiriki katika shughuli za kilimo na mifugo. Katika kipindi cha 1998/99 Wizara yangu ikishirikiana na Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma (PSRC) itaendelea kufanya marekebisho na ubinafsishaji wa mashirika ya Umma, ili tuweze kubaki na bodi za kusimamia na kudhibiti ubora wa mazao kwa niaba ya Serikali. Makampuni na Mashirika yafuatayo yamepangwa kubinafsishwa katika kipindi cha mwaka 1998/99;

(a) Viwanda vya korosho vyote

(b) Vinu vya kukobolea mpunga vya Isaka, Tabora, Shinyanga na Mwanza vilivyopo chini ya Shirika la Taifa la Usagaji - NMC.

(c) Mashamba ya Kahawa ya Mbozi, Ishera, Ndugu II, Ndugu I, Tukumbi, Ihanda na Hanseketwa.

(d) Mashamba ya ng'ombe wa nyama ya Mkata, Manyara, West Kilimanjaro, Kagoma, Dakawa, na Kalambo yaliyo chini ya National Ranching Company - NARCO.

(e) Mashamba ya NAFCO ya Mpunga ya Ruvu, Dakawa, Mbarali na Kapunga, mashamba ya mahindi ya Mbozi na Kahe na shamba la ng'ombe wa maziwa Kahe.

(f) Mashamba ya Kampuni ya Ng'ombe wa maziwa DAFCO ya Ngerengere, Kitulo, Utegi na Malonje.

(g) Kampuni ya Sukari ya Tanganyika Planting ya Moshi, Kagera Sugarna Mtibwa.

(h) Mashamba ya Ngano na Karakana yaliyoko Babati - Arusha ya Basuto, Gawal, Gidagamowd, Mulbadaw, Murjanda, Setchet, na Warret.

(i) Kiwanda cha kusindika nyama cha Tanganyika Pakers Ltd. (TPL)

(j) Mashamba/viwanda chini ya mamlaka ya chai (TTA) ambavyo ni:

- Tanzania Tea Blenders
- Mufindi Tea Co. Ltd.
- Malangali Tea Estate
- Kiwanda cha Lushoto

- Maruku/Katoke Tea Estates
- Viwanda vya Rungwe.

Aidha Wizara itaendelea kushirikiana na Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma (PSRC) katika zoezi linaloendelea la kuangalia upya miundo ya mashirika na ubinafsishaji wake, ili kwa yale yenye matatizo hasa ya ardhi, uangalifu mkubwa uchukuliwe kwa kushirikisha pia uongozi unaohusika katika maeneo hayo, ili ardhi ibakie mikononi mwa Watanzania.

## Sera na Mipango ya Kilimo na Ushirika

79. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 1998/99, Wizara yangu itaendelea kutayarisha mipango na programu za Sekta kwa kuzingatia Sera za Serikali za kijumla za uchumi na za Sekta yenyewe. **Wizara hivi sasa imekamilisha uchapishaji wa sera ili iweze kusambazwa na kusomwa na watu wengi.** Hivi sasa Wizara inakamilisha utayarishaji wa mikakati pamoja na mpango wa utekelezaji wa sera. Ili kuimarisha upatikanaji wa taarifa na takwimu ya sekta ya kilimo, Wizara ya Kilimo na Ushirika, katika muundo wake mpya imeanzisha sehemu ya ukusanyaji, uchambuaji na usambazaji wa taarifa na takwimu (Management Information System). Sehemu hiyo itashughulika na taarifa na takwimu za uzalishaji wa mazao ya kilimo na mifugo, magonjwa ya mimea na mifugo, taarifa za masoko, matokeo ya utafiti mbalimbali wa mazao na mifugo na taarifa za vyama vya ushirika. Madhumuni ya kuanzisha sehemu hii ya taarifa na takwimu za sekta ya kilimo, mifugo na ushirika ni kuiwezesha Wizara kuwa na takwimu sahihi kwa maendeleo ya kilimo, ufugaji na ushirika nchini kote ili kutoa maamuzi sahihi na kwa wakati unaofaa. Wizara yangu itaendelea kuhamasisha sekta binafsi na kuiwekea mazingira yenye kuvutia ili iweze kuwekeza katika sekta ya kilimo na mifugo.

## Mkakati wa Uwezeshaji

80. Mheshimiwa Spika, sote tunaelewa matatizo makubwa yanayokwamisha maendeleo ya sekta ya kilimo, mifugo na ushirika. Mengi ya matatizo hayo yanaambatana na uwekezaji mdogo wa mtaji katika sekta hii, huduma duni na uhaba wa mkopo kwa wakulima na wafugaji pamoja hali duni ya miundo mbinu ya vijijini (rural infrastructure) ikiambatana na matatizo ya kilimo kinachotegemea mvua. Kwa kutambua matatizo hayo niliyoyataja pamoja na mengine ambayo sikuyagusia, serikali kupitia Wizara yangu inaendelea kuhuisha mikakati ya kilimo/mifugo kwa lengo la kuwa na ile inayofaa na inayolenga kutatua matatizo hayo. Moja ya mikakati inayopendekezwa na ambayo imeanza kuchambuliwa ni mkakati wa uwekezaji na uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara, na uendelezaji wa mifugo.

81. Mheshimiwa Spika, mkakati mwingine ni ule wa “UWEZESHAJI” Empowerment kwa wananchi wenyewe kuanza kilimo na ufugaji mkubwa na wa kibiashara. Katika mpango huu, dhumuni kubwa litakuwa ni kuwezesha na kuweka mazingira mazuri yatakayowezesha Watanzania wengi wenye upeo na ujuzi wa kutosha waingie hatua ya pili ya uzalishaji wa mazao na ufugaji wa kibiashara hatimaye waweze kuanzisha usindikaji wa mazao hayo wao wenyewe. Mpango huu unatarajia kuongeza ajira kwa Watanzania, kuongeza uwezo wetu wenyewe katika kushughulikia kilimo cha kibiashara, na hatimaye kuongeza kipato cha Watanzania wengi kwa nia ya kupunguza umaskini hasa kwa kina mama wengi waishio vijijini.

82. Mheshimiwa Spika, baadhi ya miradi imeonyesha mafanikio katika baadhi ya mikoa yetu. Mfano mzuri ni miradi ya kuendeleza ng’ombe wa maziwa mikoa ya Tanga, na Kagera, **kwa utaratibu wa kopa ng’ombe lipa ng’ombe** ambayo inagharamiwa na Serikali ya Uholanzi. Lengo la miradi hii ni kuwaongezea uwezo wa uzalishaji kwa wafugaji wadogo wadogo, katika mikoa hiyo. Mfano mwingine ni mradi wa utoaji wa huduma binafsi za tiba ya mifugo kwa mabwana mifugo na waganga wa mifugo walioacha kazi au wanaotaka kujiajiri wenyewe. Nchi za Jumuiya ya Ulaya zinafadhili mpango huu. Kwa sasa Wizara inaandaa mpango wa namna ya kuzifikisha huduma hizo vijijini maana zimeenea mijini zaidi. Mradi wa kuendeleza uzalishaji miche ya kahawa wenye lengo la

kuwawezesha wakulima wenyewe wazalishe miche ya kahawa na kuipanda ili kuongeza uzalishaji mara mbili kwa miaka 5 ijayo.

83. Mheshimiwa Spika, baadhi ya nchi kama Botswana na Malaysia zimefanikiwa katika kuchukua hatua za makusudi za kuhakikisha kuwa wananchi wanapewa kila aina ya uwezo, kimtaji ili waweze kufungua mashamba makubwa ya kilimo na mifugo, kwa masharti maalum ambayo yanakuwa yameandaliwa. Kati ya masharti hayo, huwa ni kupewa vigezo vya viwango vya uzalishaji; ulipaji wa madeni yanayotokana na mikopo; kuongeza nafasi za ajira, matumizi ya teknolojia muafaka katika kilimo, kuwa na mpango mzuri wa biashara na mpango wa matumizi bora ya ardhi ili kuhifadhi ardhi na mazingira.

84. Mheshimiwa Spika, Wizara yangu imeandaa mapendekezo kadhaa Serikalini ili uanzishwe mfuko maalumu au mchango wa aina yoyote ile utakao changia jitihada hizi. Tayari Wizara yangu imekwisha tengewa shs. milioni 2.2 kutoka Serikali ya Denmark chini wa mradi ya **“Agriculture Sector Programme Support”** kwa ajili ya kuendeleza sekta binafsi ya mifugo. Vile vile shilingi milioni 2.0 zimetengwa na Benki ya Dunia, kupitia mradi wa “**Agriculture Sector Management Project**”, kwa ajili ya kuendeleza sekta binafsi ya Kilimo.

85. Mheshimiwa Spika, njia mojawapo kwa nchi yetu kuleta mageuzi katika kilimo ni kuanza mara moja mkakati wa **“Uwezeshaji”** kwa wananchi wetu kushirikishwa katika kuyamiliki baadhi ya mashamba yanayobinafsishwa ili yajibu matarajio ya wananchi na Waheshimiwa Wabunge juu ya hatma ya mashamba hayo ambayo yanabinafsishwa. Serikali ya awamu ya tatu, baada ya kutambua hili, imeamua kuliangalia upya suala zima la ubinafsishaji wa mashamba hayo ili sehemu kubwa ibakie kwa Watanzania wenye uwezo wa kuyaendesha kwa kuyagawa katika maeneo madogo (small economic sizes). Hivyo kwa mwaka 1998/99 Wizara itaweka mkazo katika yafuatayo:

(a) Kuhuisha sheria zinazokwamisha utekelezaji wa sera za kilimo, mifugo na ushirika.

(b) Kuhamasisha uundaji wa vikundi mbalimbali na vyama vya ushirika.

(c) Kushirikisha sekta binafsi katika kubuni mikakati ya kuendeleza sekta ya kilimo na mifugo.

## Nane Nane

86. Kwa kipindi cha miaka 4 mfulululizo Wizara imekuwa ikiendelea kusimamia na kuratibu sherehe za wakulima. Ili kutoa msukumo kwa washirikishwaji katika sherehe hizo, Wizara imeamua kupitia shirikisho la vyama vya ushirika kwa kushirikiana na TASO wawe wanaandaa sherehe kila mwaka kwa kuhusisha viongozi wa wilaya na vijiji. Kwa mwaka huu wa 1998 sherehe za wakulima kitaifa zilipangwa kufanyika mkoani Mwanza au Mbeya: kutokana na mikoa hii kushindwa kuadhimisha sherehe hizi, sasa zitafanyika mikoani Arusha. Wizara inapendekeza kila mkoa na kila wilaya kuandaa sherehe zao wenyewe.

## Soko Huru

87. Mheshimiwa Spika, Utekelezaji wa Sera ya Soko Huru kwa mazao ya Kilimo ya Biashara utaingia katika mwaka wake wa tano tangu sera hiyo ianze kutumika katika msimu wa 1994/95. Utekelezaji wa Soko huru kwa mazao ya Biashara na chakula umeendelea vizuri pamoja na kuwepo mafanikio, matatizo mbali mbali yamejitokeza yakiwemo ukiukaji wa kanuni na taratibu za ununuzi wa mazao, kutozingatia ubora wa mazao na vipimo, ukwepaji wa malipo ya ushuru na wakulima kukopwa mazao yao na wakati mwingine kupewa bei ndogo. Aidha kwa mazao manne ambayo yalihusishwa na sera hii katika mwaka huo wa 1994/95 (kahawa, pamba, korosho na tumbaku), mafanikio ya kuongezeka kwa uzalishaji wa kila zao yalibainika katika misimu minne ya utekelezaji wa Sera hiyo. Hali hii ya kuongezeka kwa mazao ilitokana na kuwepo kwa bei nzuri ya kuuzia nje ya nchi katika kipindi hicho cha miaka minne (1994/95 - 1997/98). Matarajio ya uzalishaji katika msimu wa 1997/98, si wa kuridhisha,

uzalishaji wa mazao haya unategemewa kushuka kutokana na athari za mvua za El-Nino. Hali hii ya kushuka kwa uzalishaji itaambatana na kushuka kwa bei za kuuzia nje za mazao haya, ambazo zitapelekea bei za wakulima nazo zishuke hapa nchini. Pamoja na hayo, tumeziagiza Bodi zote za mazao kuwa wanunuzi wote wasiruhusiwe kuwalipa wakulima bei ambayo ni chini ya asilimia sitini ya bei ya soko la dunia. Baada ya sheria na kanuni kurekebishwa, Bodi za mazao zimeagizwa kusimamia kikamilifu sheria hizo katika kudhibiti ubora wa mazao na kuhakikisha sheria zinafuatwa.

88. Mheshimiwa Spika, pamoja na mabadiliko haya ya masoko na uzalishaji yaliyojitokeza katika msimu wa 1997/98, Wizara yangu imepanga kuipanua sera hii ya soko huru kwa kuyahusisha mazao mengine matatu zaidi, yaani Chai, Pareto na Mkonge ili wakulima wa mazao hayo wafaidike na mfumo huu wa soko huru kutokana na:

(a) Ongezeko la uzalishaji kufuatia bei nzuri ya mazao.

(b) Wakulima kulipwa papo kwa papo.

(c) Ujenzi wa viwanda vya usindikaji wa mazao haya.

(d) Kuongezeka kwa wanunuzi na kuimarisha ushindani.

## IV. SHUKRANI

89. Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kuzishukuru nchi na mashirika mbalimbali ya Kimataifa yanayoendelea kuisaidia Wizara yangu katika juhudi za kuendeleza kilimo, mifugo na ushirika. Napenda kwanza kuzishukuru nchi za Australia, Canada, China, Denmark, Finland, India, Indonesia, Ireland, Italia, Japan, Korea ya Kaskazini, Korea Kusini Marekani, New-Zealand, Norway, Ubelgiji, Ufaransa, Uholanzi, Uingereza, Ujerumani, Uswisi, Sweden na Thailand. Vile vile Mashirika na Taasisi za Kimataifa kama ifuatavyo: Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, UNDP, FAO, EU, UNICEF, SADC, WFP, IFAD, CFTC, CILCA, CIMMYT, EADB, HPI, ICRAF, ICRISAT, IDRC, IITA na Sasakawa Global 2000. Bado tunahitaji misaada yao ili tuweze kuendeleza kilimo chetu nchini.

90. Mheshimiwa Spika, napenda kutoa shukrani za pekee kwa Wakulima na Wafugaji wa nchi hii kwa kazi kubwa wanayoifanya, katika uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara. Aidha napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao, ambayo imeiwezesha Wizara yangu kutekeleza mambo mengi kwa ufanisi mkubwa kwa nia ya kuwaendeleza wakulima na wafugaji nchini. Pia napenda kumshukuru Naibu Waziri Mheshimiwa Profesa Pius Mbawala, Katibu Mkuu wa Wizara Luteni Kanali Tirumanywa Philibert Magere pamoja na Wafanyakazi wote wa Wizara na Mashirika yote yaliyochini ya Wizara yangu kwa kazi nzuri waliyoifanya pamoja na hali ngumu waliyokumbana nayo katika kutekeleza majukumu ya Wizara. Aidha napenda kutoa shukrani za pekee kwa Mheshimiwa Njelu Kasaka - Mkuu wa mkoa wa Iringa, ambaye ametoa mchango mkubwa katika kuendeleza sekta ya kilimo na mifugo wakati akiwa Naibu Waziri wa Wizara hii. Mimi binafsi napenda kumtakia heri katika kazi yake mpya ya kusimamia maendeleao ya mkoa wa Iringa, hasa utekelezaji wa shughuli za kilimo, mifugo na ushirika. Wizara yangu itampatia kila aina ya msaada katika utendaji wake wa kazi za kila siku. Mwisho natoa shukrani kwa Mpiga chapa Mkuu wa Serikali kwa kazi nzuri ya kuchapa hotuba hii.

## V. MAOMBI YA FEDHA 1998/99

93. Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya, nina amini kuwa Waheshimiwa Wabunge watapenda kutoa ushauri, maoni na maelekezo ya jinsi ya kuboresha utendaji ndani ya Wizara yangu. Ili niweze kutekeleza hayo ninayokusudia kuyafanya kwa mwaka huu wa fedha, naomba Bunge lako Tukufu liidhinishe shilingi milioni

15,316.6 kwa ajili ya matumizi ya kawaida, na shilingi milioni 21,850.2 kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Kati ya fedha hizi za maendeleo, shilingi milioni 1,000.0 ni fedha za hapa na shilingi milioni 20,850.2 ni za nje.

94. Mheshimiwa Spika, na Waheshimiwa Wabunge nawashukuru kwa kunikubalia na kunisikiliza katika hoja yangu hii.

95. **Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.**